

**MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA
TAIFA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA YA
MWAKA 2017 KWA KIPINDI CHA MWAKA
2017/18 - 2027/28**

OKTOBA, 2017





YALIYOMO

YALIYOMO	iii
UFUPISHO WA MANENO	vi
UFAFANUZI WA ISTILAHU	ix
SURA YA KWANZA.....	1
MAELEZO YA AWALI	1
1.1 Utangulizi wa Utekelezaji wa Mkakati	1
1.2 Masuala ya Utekelezaji	1
1.3 Mgawanyo wa Majukumu kwa Taasisi na Wadau mbalimbali	1
1.4 Matokeo yanayotarajiwa kwa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017.....	2
1.5 Hitimisho	2
SURA YA PILI	3
UCHAMBUZI WA HALI ILIVYO KATIKA SEKTA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA TANZANIA	3
2.1 Mapitio ya Mwenendo wa Uchumi	3
2.2 Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000.....	4
2.2.1 Mafanikio ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000	4
2.2.2 Vikwazo Wakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000	9
2.2.3 Athari Zilizojitokeza wakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000.....	12
2.2.4 Changamoto Zilizojitokeza katika Kutekeleza Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000	13
2.3 Umuhimu wa Kufanya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000	15

SURA YA TATU.....	18
DIRA, DHIMA NA MALENGO.....	18
3.1 Dira	18
3.2 Dhima	18
3.3 Malengo ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017.....	18
3.3.1 Lengo Kuu	18
3.3.2 Malengo Mahsusi.....	18
SURA YA NNE.....	20
UTEKELEZAJI WA HOJA, MALENGO, MIKAKATI NA SHABAHA YA SERA YA TAIFA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA.....	20
4.1 Huduma Jumuishi za Fedha	20
4.2 Uendelevu wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha.....	23
4.3 Usimamizi wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha.....	25
4.4 Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Huduma za Sekta Ndogo ya Fedha	27
4.5 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa	28
4.6 Utawala Bora katika Sekta ndogo ya fedha	29
4.7 Makundi yenye Mahitaji Maalum, Jinsia na Vijana.....	31
SURA TANO.....	33
BANGO KITITA LA MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA YA MWAKA, 2017	33
SURA YA SITA	58
WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU WAKUU	58
6.1 Wajibu na Majukumu ya wadau wa Huduma Ndogo za Fedha.....	58
SURA YA SABA.....	66
MFUMO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI	66
7.1 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini.....	66

7.2	Malengo na miongozo ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini	67
7.3	Wigo wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini	67
	7.3.1 Viashiria vya utekelezaji	67
7.4	Ukusanyaji na Uchambuzi wa Takwimu	75
	7.4.1 Aina ya taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini.....	76
	7.4.2 Ratiba ya Utoaji Taarifa	76
	7.4.3 Mtiririko wa Utoaji Taarifa.....	78
	7.4.4 Mfumo wa Utoaji Mrejesho	79
7.5	Matumizi ya Taarifa za Tathmini na Ufuatiliaji.....	79
7.6	Mpango wa Utekelezaji	79

UFUPISHO WA MANENO

AfDB	African Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Afrika)
AgFiMS	Agricultural Finance Markets Scoping (Utafiti wa Masoko ya Fedha kwa Ajili ya Kilimo).
AML	Anti-Money Laundering (Udhibiti wa utakatishaji ya Fedha Haramu)
ASCAs	Accumulative Savings and Credit Associations (Ushirika wa Kuweka Akiba na Mikopo)
ATMs	Automated Teller Machines (Mashine za kielektoniki za Kutolea Fedha)
BAFIA	Banking and Financial Institutions Act (Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha)
BDS	Business Development Services (Huduma za Kuwezesha Maendeleo ya Biashara)
BOT	Bank of Tanzania (Benki Kuu ya Tanzania)
CBOs	Community Based Organisations (Mashirika ya Kijamii)
CFG's	Community Financial Groups (Vikundi vya Kifedha vya Kijamii)
CFT	Combating Financing of Terrorism (Kubambana na Ufadhili wa Ugaidi)
CMSA	Capital Markets and Securities Authority (Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana)
CRB	Credit Reference Bureau (Chombo cha Kubadilishana Taarifa za Wakopaji)
CSA	Cooperative Societies Act (Sheria ya Vyama vya Ushirika)
DOE-UDSM	Department of Economics of the University of Dar es Salaam Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)
ESRF	Economic and Social Research Foundation (Taasisi ya Uchumi na Utafiti wa Kijamii)
EAMU	East Africa Monetary Union (Umoja wa fedha wa Afrika Mashariki)
ECGS	Export Credit Guarantee Scheme (Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Mauzo Nje ya Nchi)
FICOS	Financial Cooperative Societies (Vyama vya Ushirika wa Fedha)

FIs	Financial Institutions (Taasisi za Fedha)
FSDT	Financial Sector Deepening Trust (Mfuko wa Udhamini wa Sekta ya Fedha)
GDP	Gross Domestic Product (Pato la Ndani la Taifa)
ICT	Information and Communication Technology (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano)
IFAD	International Fund for Agriculture Development (Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo wa Kimataifa)
MALF	Ministry of Agriculture, Livestock and Fisheries (Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi)
MFAEAIC	Ministry of Foreign Affairs and East Africa Cooperation (Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki)
MFI	Microfinance Institutions (Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha)
MoHCDEC	Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto)
MITI	Ministry of Industry, Trade and Investment (Wizara ya Viwanda, Biashara, na Uwekezaji)
MIVARF	Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance (Mpango wa Kuboresha Miundombinu ya Masoko, Kuongeza Thamani na Huduma za Fedha Vijijini)
MLHHS	Ministry of Land, Housing and Human Settlements (Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi)
MNOs	Mobile Network Operators (Watoa Huduma kwa Njia ya Mtandao wa Simu)
MOFP	Ministry of Finance and Planning (Wizara ya Fedha na Mipango)
MoEVT	Ministry of Education and Science and Technology (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia)
MSMEs	Micro, Small and Medium Enterprises (Wajasiriamali Wadogo na wa Kati)
NBS	National Bureau of Statistics (Ofisi ya Taifa ya Takwimu)
NEDF	National Entrepreneurs Development Fund (Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali)
NEEC	National Economic Empowerment Council (Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi)

NGOs	Non-Governmental Organizations (Asasi Zisizo za Serikali)
NMP	National Microfinance Policy (Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha)
PHC	Population and Housing Census (Sensa ya Watu na Makazi)
PPF	Parastatal Pensions Fund (Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma)
PTF	Presidential Trust Fund (Mfuko wa Rais wa Kujitegemea)
ROSCAS	Rotating Savings and Credit Associations (Ushirika wa Akiba na Mikopo kwa Zamu)
SACCOS	Savings and Credit Cooperative Societies (Vyama vya Ushirika Kuweka Akiba na Mikopo)
SELF MF	SELF Microfinance Fund (Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha wa SELF)
SDGs	Sustainable Development Goal (Malengo ya Maendeleo Endelevu)
SSRA	Social Security Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii)
TCDC	Tanzania Cooperative Development Commission (Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania)
TCRA	Tanzania Communication Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania)
TDHS	Tanzania Demographic and Health Survey (Utafiti wa Afya na Demografia Tanzania)
TIC	Tanzania Investment Centre (Kituo cha Uwekezaji Tanzania)
TIRA	Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania)
TPSF	Tanzania Private Sector Foundation (Taasisi za Sekta Binafsi Nchini Tanzania)
URT	United Republic of Tanzania (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
VICOBA	Village Community Bank (Benki ya Jamii Vijijini)
VSLA	Village Savings and Loans Association (Chama cha Kuweka Akiba na Mikopo Vijijini)
YDF	Youth Development Fund (Mfuko wa Maendeleo ya Vijana)

UFAFANUZI WA ISTILAHU

“Akiba ya Hiari” ni jumla ya fedha ambazo zimewekwa kwa hiari na mteja wa huduma ndogo za fedha (na sio kwa masharti ya kupata mkopo) ambazo anaweza kuchukua wakati wowote.

“Akiba ya lazima” ni asilimia/ sehemu ya fedha ya mteja wa taasisi ndogo za fedha zinazowekwa kwenye benki au taasisi za fedha kama akiba yake kwenye kikundi kabla ya kupata mkopo wa kwanza au unaofuatia au yote kwa pamoja.

“Amana” ni fedha inayoweza kutolewa baada ya kuwekwa na mteja kwa masharti ya kupata riba/faida kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa kwenye hati ya amana na ambayo inaweza kutumika kama dhamana wakati wa kukopa.

“Benki Zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha” ni taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha ambazo zimepewa leseni na Benki Kuu ya Tanzania kufanya biashara ya benki kwa mtu binafsi, vikundi, wajasiriamali wadogo na wa kati wenye kipato cha chini katika maeneo ya vijijini au mijini.

“Biashara ya Fedha” ni mikopo, kuwekeza au kuweka fedha au dhamana au vyote viwili, kupokea, kupata au kununua kutoka katika umma au kutoka kwa kikundi cha watu kwa njia ya amana, kukopa, michango, tozo au kutoka kwenye hesabu ya mtu aliyepokea fedha au dhamana au kutoka kwenye hesabu za watu wengine.

“Chama kilele” Ni shirikisho la vyama vya watoa huduma ndogo za fedha lenye lengo la kushawishi na kutetea maslahi ya wanachama katika sekta ndogo ya fedha

“Chombo cha ubadilishanaji wa taarifa za mikopo” ni chombo maalum kilichoundwa kwa ajili ya kukusanya na kuhifadhi taarifa mbalimbali zinazohusiana na malipo ya mikopo, hukumu za mahakama, kufilisika kwa wakopaji na kupata taarifa za wakopaji wa rasilimali za umma (binafsi na makampuni) na kuuza taarifa hizo kwa watumiaji.

“Dhamana” ni mali zilizoahidiwa na mkopaji kwa mkopeshaji kwa ajili

ya kulinda mkopo hadi utakaporejeshwa. Endapo mkopaji atashindwa kulipa mkopo kama alivyoahidi, mkopeshaji atakuwa na haki ya kuchukua na kuuza dhamana ili kulipa deni.

“Elimu ya Fedha” ni elimu ya masuala ya fedha ambayo inatolewa kwa lengo la kutoa fursa ya kuchagua huduma bora za fedha ili kufikia lengo la huduma ya fedha iliyochaguliwa kwa ajili ya ustawi wa jamii.

“Huduma Jumuishi za Fedha” ni utaratibu wa kuhakikisha upatikanaji na utumiaji wa huduma za fedha kwa wananchi wenye kipato cha chini kwa kutumia miundombinu ya mifumo ya malipo yenye gharama nafuu kwa haki na uwazi na kwa kushirikisha taasisi husika.

“Huduma Ndogo za Bima” ni huduma za bima zinazolenga wananchi wenye kipato cha chini ili kuwakinga dhidi ya athari za majanga kama vile ajali, maradhi, vifo na majanga ya asili kulingana na malipo yatakayotolewa, mapato na kiwango cha athari.

“Huduma Ndogo za Fedha kwa ajili ya makazi” ni utoaji wa mikopo midogo isiyo na dhamana, ambayo inaambatana na huduma nyingine za fedha kama vile uwekaji wa akiba, kutuma fedha na huduma ndogo za bima ili kukidhi mahitaji ya kaya zenye kipato cha chini kwa ajili ya kukarabati au kuimarisha makazi au kujenga nyumba.

“Huduma Ndogo za Fedha” ni huduma ndogo za fedha zitolewazo kwa wananchi wa kipato cha chini (mtu binafsi, kaya, na kikundi cha ujasiriamali) ambao hawajafikiwa na mfumo rasmi wa fedha zikiwemo huduma ndogo za mikopo ya karadha, nyumba, bima, akiba, pensheni, kuhaulisha fedha, elimu ya fedha na ujasiriamali.

“Huduma Ndogo za Fedha za kielektroniki” ni utoaji wa huduma ndogo za fedha kwa njia ya mtandao wa kielektroniki.

“Huduma ya Kuendeleza Biashara” ni huduma zisizo za fedha zinazotolewa kwa wateja wa huduma ndogo za fedha katika hatua mbalimbali kulingana na mahitaji ya wateja hao kwa lengo la kuongeza ujuzi na ushauri wa kibiashara kwa vikundi mbalimbali.

“Kampuni ya Huduma Ndogo za Fedha” ni taasisi ya fedha iliyoanzishwa kwa sheria ya kampuni yenye dhima na ukomo wa hisa kwa ajili ya kutoa huduma ndogo za fedha isipokuwa biashara ya benki kwa wateja wa huduma ndogo za fedha kama ilivyotafsiriwa.

“Karadha/ Mikopo ya Vifaa” ni mikopo inayotolewa kwa wananchi wa kipato cha chini kwa njia ya vifaa yenye sifa zifuatazo (i) thamani ya wastani wa mali katika orodha ya fedha zilizowekwa kwa faida ni hadi shilingi za Tanzania milioni kumi (ii) muda wa kukodisha hauzidi miezi 24.

Kumlinda Mlaji” ni kanuni na taratibu zilizoandaliwa kwa ajili ya kuwalinda wateja/walaji wapatapo huduma za fedha kwa watoa huduma hizo ili kuhakikisha kuwa huduma zinatolewa kwa uaminifu, uwazi na usawa kwa manufaa ya umma.

“Kundi la watu wenye Kipato cha Chini” ni kundi la watu wenye kiwango cha chini cha kipato kama inavyoainishwa kwenye taarifa za mara kwa mara kulingana na mazingira ya nchi.

“Kupanuka kwa Huduma za Fedha” ni utaratibu wa kuongezeka na kusambaa kwa watoa huduma za fedha na watumiaji wake ndani ya mfumo wa fedha.

“Masoko ya Mitaji” ni sehemu ya mfumo wa fedha ambao unawezesha uhamasishaji wa upatikanaji wa mitaji kwa njia ya dhamana au mikopo kwa ajili ya kuwezesha shughuli za kiuchumi.

“Mfumo wa Malipo” ni utaratibu unaojumuisha nyenzo za malipo, taratibu za kibenki au za kuhaulisha fedha kati ya benki moja na nyingine au baina ya watoa huduma ya mfumo wa malipo ambao unahakikisha mzunguko wa fedha kwa mujibu wa idhini itolewayo chini ya Sheria ya Mfumo wa Malipo ya Taifa, 2015.

“Mikopo Midogo” ni mikopo ya kiwango cha chini inayotolewa kwa wananchi wa kipato cha chini ambao hawafikiwi na huduma za fedha, au itakavyobainishwa na msimamizi.

“Mtandao au shirikisho” ni taasisi/asasi zinazoundwa kwa mlengo mmoja kwa ajili ya uzengezi na ushauri katika masuala yanayohusiana na huduma ndogo za fedha kwa Serikali au mamlaka za udhibiti kwa niaba ya wanachama.

“Mteja wa Huduma Ndogo za Fedha” ni mtu binafsi, kikundi au wajasiriamali ambao wanapata na kutumia huduma kutoka kwa watoa huduma ndogo za fedha.

“Mtoa Huduma kwa njia ya Mtandao wa Simu” ni mtoa huduma za mawasiliano ya kielektroniki isiyotumia nyaya ambaye anamiliki au kudhibiti vifaa vyote muhimu katika kuuza na kutoa huduma kwa mtumiaji wa mwisho ikiwa ni pamoja na mgao wa masafa ya redio, miundombinu ya mtandao isiyotumia nyaya, kutoa ankara, huduma kwa wateja, mfumo wa kompyuta, masoko na ukarabati.

“Mtoa Huduma Rasmi za Fedha” ni Mtu/taasisi ambayo hutoa huduma za fedha ambayo imesajiliwa rasmi, yenye leseni na inasimamiwa na mamlaka ya udhibiti.

“Mtoa Huduma ya Mfumo Malipo” ni shirika linalojishughulisha pekee yake au kwa kushirikiana na shirika lingine katika kutoa huduma ya malipo ya kielektroniki iliyoidhinishwa na sheria ya Taifa ya Mifumo ya Malipo, 2015.

Mtoa huduma za Kuendeleza Biashara ni taasisi zisizo za kifedha ambazo huwawezesha wateja au watoa huduma ndogo za fedha kwa kuwapa ujuzi wa biashara kwa kutumia mbinu mbali mbali hususan miongozo, mafunzo, usimamizi na ushauri elekezi.

“Shirikisho/Mtandao wa Watoa Huduma ndogo za Fedha” ni chombo cha juu cha watoa huduma ndogo za fedha.

“Taasisi ya huduma Ndogo za Fedha” ni taasisi iliyoanzishwa kwa lengo la kutoa huduma ndogo za fedha kwa wateja wa taasisi hizo kama inavyotafsiriwa.

“Taasisi za Fedha” ni taasisi inayojishughulisha na biashara ya benki, yenye ukomo wa mtaji, eneo au shughuli zilizoruhusiwa kufanywa na

taasisi hiyo kama ilivyoelezwa kwenye sheria ya Benki Kuu ya Tanzania au masharti mengine yanayoambatana na leseni.

“Udhamini wa kikundi” ni mkataba kati ya vikundi vya wakopaji wa huduma ndogo za fedha ambao unawaunganisha pamoja au baadhi yao kwa lengo la kuhakikisha mikopo waliochukua inalipwa.

“Ujasiriamali Mdogo” ni biashara ndogo zinazofanywa na mtu mmoja au familia zilizo katika sekta isiyo rasmi, haina mfumo wa kuhifadhi taarifa za fedha na mali zake haziwezi kutumika kama dhamana ya mikopo.

“Utakatishaji wa Fedha Haramu” ni ushiriki wa moja kwa moja au vinginevyo wa mtu mmoja au zaidi katika kubadili, kuhamisha, kuficha, kudanganya, kutumia au kumiliki fedha au mali inayojulikana kuwa haramu na ambapo ushiriki huo unalenga kuepuka matokeo ya hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na makosa yaliorejewa katika Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura. 423.

“Uwakala wa huduma za Benki” Ni biashara inayohusu kutoa huduma za kibenki kwa wateja kwa niaba ya taasisi ya benki husika kwa mkataba halali wa uwakala na taasisi hiyo.

“Vikundi vya Kifedha vya Kijamii” ni kikundi kilichoundwa kwa lengo la kutoa huduma ndogo za fedha ambacho kinamilikiwa na kusimamiwa na wanachama wenyewe. Vikundi hivi vinahamasisha kuweka akiba kwa mtu mmoja mmoja na kutoa mikopo ya muda mfupi kwa wanachama, huduma ndogo za bima, na wakati mwingine kwa wasio wanachama katika viwango vya riba tofauti kwa kutegemeana na muundo wao.

“Wasiopata huduma za fedha” ni wananchi ambao wanajishughulisha kiuchumi lakini hawajafikiwa na huduma zinazotolewa na taasisi rasmi za fedha.

“Watoa Huduma ndogo za Fedha” ni taasisi/asasi inayojishughulisha na biashara ya kutoa huduma ndogo za fedha.



SURA YA KWANZA

MAELEZO YA AWALI

1.1 Utangulizi wa Utekelezaji wa Mkakati.

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 kwa ufanisi, Unahitaji mkakati mahsusi. Mkakati huu wa utekelezaji utatilia mkazo malengo na matamko ya sera yapewe kipaumbele ili yafanikishwe ndani ya muda wa miaka 10 kuanzia 2017 hadi 2027.

Mkakati utatoa mpango wa utekelezaji; utataja rasilimali na mikakati ya upatikanaji wake kwa Serikali kupitia wizara inayohusika na masuala ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017. Mkakati wa utekelezaji utaoanishwa na mipango na programu mbalimbali za sekta ya fedha ili kuleta matokeo yenye manufaa kwa sekta ya fedha kwa ujumla.

1.2 Masuala ya Utekelezaji

Maeneo ambayo yamepewa kipaumbele na kuainishwa katika Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 ni: kuanzisha mfumo mahsusi wa kitaasisi; kutunga sheria madhubuti inayoendana na mienendo ya soko; kushughulikia masuala yanayovuka mipaka ya nchi; na kuzingatia viwango bora vya utendaji.

1.3 Mgawanyo wa Majukumu kwa Taasisi na Wadau mbalimbali.

Watekelezaji wakuu wa mkakati huu ni kutoka taasisi za Serikali kama vile Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania na wadau wengine katika sekta ndogo ya fedha.

Wizara ya Fedha na Mipango na wadau wengine wakuu wamepewa majukumu kama njia ya kuhakikisha utekelezaji unafanyika kwa ufanisi. Inatarajiwa kwamba mkakati wa utekelezaji utasaidia kufanikisha kwa ufanisi malengo ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017.

1.4 Matokeo yanayotarajiwa kwa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017

Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 itaweka mazingira mazuri yatakayohamasisha maendeleo ya ubunifu wa huduma ndogo za fedha zitakazokidhi mahitaji halisi ya makundi ya kipato cha chini kwa lengo la kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Aidha, sera itaweka uratibu mzuri, usimamizi na mfumo wa sheria kwa masuala ya sekta ndogo ya fedha nchini. Vilevile, Sera itaendelea kutumika kama mwongozo kwa wadau wote na hivyo kuchochea uanzishwaji wa taasisi mpya za fedha na zilizopo kukua na kuongeza ushindani. Sera hii itatoa mwongozo na kuwataarifu wadau wote katika kuendeleza masuala mbalimbali ya sekta ndogo ya fedha. Matokeo ya utekelezaji wa mkakati kwa kiasi kikubwa utaongeza; utaratibu rasmi, utamaduni wa kuweka akiba, ustawi wa sekta ndogo za fedha, kupunguza umaskini, ukuaji wa uchumi na kazi zenye staha.

1.5 Hitimisho

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 utahakikisha huduma bora za fedha zinatolewa kwa wananchi wenye kipato cha chini ambao hawajafikiwa na huduma rasmi.

SURA YA PILI

UCHAMBUZI WA HALI ILIVYO KATIKA SEKTA NDOGO YA FEDHA

2.1 Mapitio ya Mwenendo wa Uchumi

Uchumi wa Tanzania umekua kwa kasi ambapo Pato la Taifa limekuwa likiongezeka kwa wastani wa asilimia 6.4 kwa kipindi cha muongo mmoja. Ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.0 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2010 kwa bei za mwaka 2007. Vile vile, pato la wastani la mtu kwa bei ya mwaka husika limekuwa likiongezeka katika kipindi cha miaka kumi iliyopita kutoka shilingi 276,741 mwaka 2001 hadi shilingi 1,724,416 mwaka 2014. Hata hivyo, kuna tofauti kubwa katika pato la wastani la mtu kati ya mikoa ya Tanzania Bara ambapo Dar es Salaam ikiwa na kiwango cha juu cha shilingi 2,797,694 na Singida ikiwa na kiwango cha chini cha shilingi 1,023,631 kwa mwaka 2014. Katika kipindi hicho, sekta ya fedha ilijielekeza zaidi katika utoaji rasilimali fedha kwa sekta mbalimbali za uzalishaji kiuchumi. Mwaka 2014, kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika sekta ya fedha ilipungua hadi asilimia 10.8 kutoka asilimia 19.1 mwaka 2006. Pamoja na kupungua kwa kasi hiyo, mchango wake kwenye Pato la Taifa uliongezeka na kuwa asilimia 3.4 mwaka 2014 kutoka uwiano wa asilimia 2.4 mwaka 2005.

Kulingana na taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, wastani wa mfumuko wa bei kwa mwaka kwa Tanzania Bara umekuwa na mwenendo wa kupungua tangu mwaka 2012 kwa kiwango cha asilimia 8.9 kwa mwaka. Mwaka 2015, mfumuko wa bei ulipungua hadi asilimia 5.6 kutoka kiwango cha asilimia 16.0 katika mwaka 2012. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulitokana na kupungua kwa bei za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Mwenendo huu ulichangiwa pia na hali nzuri ya hewa, kupungua kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia na sera madhubuti za kodi na fedha.

Kutokana na jitihada za kukabiliana na uchumi, hati fungani zimepanda kutoka asilimia 11.4 kwa Desemba 2007 hadi asilimia 18.25 kwa Desemba 2015. Kwa upande wa uhamasishaji kwenye uwekaji wa amana, viwango

vingi vya riba vilivyotolewa na benki za biashara vilikuwa na mwenendo wa kuongezeka. Riba za amana ziliongezeka hadi kufikia asilimia 3.42 Desemba 2015 ikilinganisha na asilimia 2.67 Desemba 2007 ambapo viwango vya riba za amana za muda maalum kwa ujumla ziliongezeka kutoka asilimia 8.37 mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 9.22 Desemba 2015. Pia, upande wa mikopo, viwango vya riba za mikopo kwa ujumla viliongezeka kutoka asilimia 15.3 Desemba 2007 hadi kufikia asilimia 16.41 Desemba 2015. Kutokana na mwenendo huo, tofauti kati ya riba za amana na mikopo iliongezeka kutoka wastani wa asilimia 6.93 Desemba 2007 hadi wastani wa asilimia 7.19 Desemba 2015.

Kulingana na taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu, wastani wa kiwango cha uhaba wa ajira ulipungua kutoka asilimia 11.7 mwaka 2007 hadi asilimia 10.7 mwaka 2011. Katika kipindi cha kati ya mwaka 2001 na 2011, wastani wa kiwango hiki ulikuwa asilimia 11.88 ambapo kiwango cha juu kabisa kilifikia asilimia 12.90 mwaka 2001 na kiwango cha chini kabisa kilikuwa asilimia 10.70 mwaka 2011.

Pamoja na viashiria vya ukuaji wa uchumi, kama ilivyo kwa nchi nyingi zinazoendelea, Tanzania inakabiliwa na changamoto kadhaa za kupunguza umaskini. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2012 (ulionesha kuwa kiwango cha umaskini kimepungua kwa asilimia 1.04 ya kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2007 hadi 2012, wakati wastani wa Pato la Taifa la kila mwaka limeongezeka kwa asilimia 6.4 kwa kipindi cha miaka kumi (10) iliyopita. Aidha, matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa asilimia 28.2 ya watanzania ni maskini na kati ya hao asilimia 9.7 wana umaskini uliokithiri.

2.2 Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000

2.2.1 Mafanikio ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000 umechangia ongezeko la watoa huduma ndogo za fedha,

namna ya utoaji wa huduma ndogo za fedha, uboreshaji wa huduma, na ushiriki wa taasisi zisizo za fedha ikiwa ni pamoja kampuni za simu kama vile Vodacom, Airtel, Tigo, Zantel na Halotel kwa kuwa na ubunifu wa kutumia teknolojia. Kwa sasa, sekta ndogo ya fedha nchini inajumuisha aina mbili za watoa huduma za fedha: (i) watoa huduma rasmi wa huduma ndogo za fedha kama benki na taasisi za fedha; vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa; kampuni za huduma ndogo za fedha, asasi za fedha zisizo za serikali, Mifuko na Programu za Serikali; na (ii) Taasisi za fedha zisizo rasmi kama vile Asasi za Kijamii, Vikundi vya Kifedha vya Kijamii (Benki za Kijamii za Vijiji (VICOBA), Ushirika wa Kuweka Akiba na Kukopa Vijijini (VSLAs), Ushirika wa Kuweka Akiba na Kukopa kwa Zamu (ROSCAs), wakopeshaji binafsi na wengine wanaotoa huduma zinazohusiana na fedha.

Kutokana na utafiti wa *FinScope* uliofanyika mwaka 2017, asilimia 16.7 ya nguvu kazi walipata huduma za benki ikilinganishwa na asilimia 9.1 mwaka 2006, wakati huo asilimia 48.6 walipata huduma za fedha kutoka kwa taasisi zisizo za benki kama vile taasisi ndogo za fedha, kampuni za bima, vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa na asasi zisizo za Serikali za fedha pamoja na huduma za malipo kwa njia za simu ikilinganishwa na asilimia 6.7 katika mwaka 2006. Vilevile, asilimia 6.7 walihudumiwa na taasisi za fedha zisizo rasmi kama vile benki za kijamii za vijiji (VICOBA), ushirika wa akiba na mikopo vijijini (VSLAs), ushirika wa kuweka akiba na kukopa kwa zamu (ROSCAs), wakopeshaji binafsi na asasi za kijamii za kuweka na kukopa pamoja na ndugu na marafiki, ikilinganishwa na asilimia 35.1 mwaka 2006. Hali kadhalika, ongezeko la watoa huduma limejidhihirisha kwenye taasisi zinazosimamiwa na zisizosimamiwa kama ifuatavyo:

(i) Benki na Taasisi za Fedha

Idadi ya benki na taasisi za fedha imeongezeka kutoka 31 mwezi Machi, 1999 hadi 63 mwezi Desemba, 2015 (benki za biashara 36, benki za ushirika na mikoa 12, taasisi za fedha 3, benki za huduma ndogo za fedha 3, taasisi za fedha

za maendeleo 2, Taasisi ya Mikopo ya Nyumba Tanzania 1, taasisi za karadha 3, benki wakilishi 1 na vituo vya ubadilishaji taarifa za wakopaji 2). Kati ya benki 56 zilizopo, benki 22 zinatoa huduma ndogo za fedha zikijumuisha benki za biashara 8, benki za huduma ndogo za fedha 3 na benki za wananchi na ushirika 11. Benki za biashara kama vile, benki ya NMB, CRDB na Akiba zimejielekeza kutoa huduma maeneo ya vijijini ili kutoa mikopo ya jumla katika maeneo hayo. Aidha, Benki ya Posta Tanzania ina mtandao wa ofisi za posta ulioenea nchi nzima ambao umewezesha uhamasishaji wa uwekaji akiba na uhaulishaji wa fedha. Vilevile, kuna benki chache za wananchi na taasisi za fedha zisizo benki ambazo zinajihusisha kupokea amana katika uendeshaji wa huduma ndogo za fedha.

(ii) Taasisi za Fedha Zisizo Benki

Taasisi za fedha zisizo benki ni pamoja na kampuni za bima, kampuni ndogo za karadha, kampuni za mikopo midogo ya nyumba, skimu za uwekezaji wa pamoja, Vyama vya Ushirika wa Kuweka Akiba na Kukopa, asasi zisizo za Serikali za fedha, kampuni za huduma ndogo za fedha, watoa huduma za mifumo ya malipo, wawekezaji binafsi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Usajili wa taasisi hizi hufanyika kupitia mamlaka na sheria mbalimbali ikijumuisha Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni; Sheria ya Taifa ya Mifumo ya Malipo ya mwaka 2015; Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013; Sheria ya Kampuni ya mwaka 2002; Sheria ya Vyama vya Kijamii Sura Na. 337 ya mwaka 1954; Sheria ya Asasi zisizo za Serikali ya mwaka, 2002; Sheria ya Udhamini Sura Na. 318 ya mwaka 2002. Taasisi hizi zinatekeleza jukumu kubwa la kutoa huduma za fedha kwa watu wa kipato cha chini na kati.

Idadi ya taasisi hizi zimeongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka kumi na tano iliyopita. Matalani, mwaka 2000, vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa

vimeongezeka kutoka 803 vikiwa na wanachama 133,134 waliowekeza hisa, akiba na amana zenye thamani ya shilingi bilioni 14.04 hadi kufikia vyama 4,093 vyenye wanachama 733,876 waliowekeza shilingi bilioni 377.6 mwaka 2015.

Vile vile, asasi zisizo za serikali za fedha na kampuni za huduma ndogo za fedha ziliongezeka kutoka tisa (9) mwaka 2002 hadi kufikia zaidi ya 292 mwaka 2016. Aidha, Mifuko ya hifadhi ya jamii imeongezeka kutoka sita mwaka 2000 hadi mifuko saba mwaka, 2016 ambayo baadhi hutoa mikopo ya jumla kwa vyama vya kuweka akiba na kukopa vya wafanyakazi kwa lengo la kukopeshana. Kwa upande wa soko la mitaji, mifuko ya uwekezaji wa pamoja ilianzishwa kwa lengo la kutoa fursa kwa wananchi wa kipato cha chini kuwekeza katika masoko ya mitaji. Hadi kufikia Desemba 2015, Mifuko hiyo ilikuwa na jumla ya shilingi bilioni 246.58

(iii) Mifuko na Programu za Serikali.

Serikali ilianzisha Mifuko na Programu mbalimbali za mikopo ili kukidhi mahitaji ya mitaji kwa wananchi wenye kipato cha chini. Baadhi ya mifuko na programu za Serikali ni pamoja: Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na programu za kuongeza ajira, mfuko wa huduma ndogo za fedha wa SELF, mfuko wa maendeleo ya vijana na wanawake, mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali, Mfuko wa Rais (PTF), mfuko wa udhamini wa Mauzo nje ya Nchi na Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Wajasiriamali wadogo na wa kati. Katika kipindi hicho, Mifuko na programu za Serikali zimewezesha kujenga uwezo na kutoa mikopo nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini. Katika kipindi kilichoishia Mei, 2015 kiasi cha shilingi bilioni 50.6 zilitolewa na kukopeshwa kwa wajasiriamali 74,790. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na mifuko ya hifadhi ya jamii iliidhinisha shilingi bilioni 105 kwa ajili ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo 256,602.

(iv) Huduma za Fedha kwa Njia ya Simu

Ubunifu katika mifumo ya malipo umewezeshwa huduma za malipo kwenye benki na taasisi zisizo za benki kutolewa kupitia simu za kiganjani. Matumizi haya ya simu yamewezeshwa kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma za fedha hususan huduma za malipo (kati ya mtu na mtu) kwa wananchi wengi ambao hawajafikiwa na huduma za benki. Huduma hizi zilianza kutolewana kampuni ya Vodacom (M-Pesa) mwaka 2008 na baadaye kampuni za Airtel (Airtel Money), Tigo (Tigo Pesa), Zantel (Ezy-Pesa) na Halotel (Halo-Pesa) zilianzisha huduma hizo. Huduma za fedha zinazotolewa kupitia simu za kiganjani zina mchango mkubwa katika jamii na uchumi kwa kuwezesha kufanyika miamala ya malipo na wakati mwingine kutunza bakaa la miamala kwenye akaunti ya kielektroniki.

Idadi ya kadi za simu zilizosajiliwa imeongezeka kutoka 360,740 Juni, 2009 hadi kufikia 49,356,465 Desemba 2015. Vile vile, bakaa iliyopo kwenye akaunti ya udhamini imeongezeka kutoka shilingi bilioni 3.05 Juni, 2009 hadi shilingi bilioni 583.8 Desemba, 2015. Kufikia Desemba, 2015 jumla ya Benki 13 zilikuwa zinatoa huduma ya uwakala wa kuweka akiba na mikopo midogo kupitia simu za kiganjani ambapo mawakala 1,719 walikuwa na amana za shilingi milioni 1,180,440.8. Katika kipindi hicho, aina mbili mpya za huduma kwa waweka akiba na wakopaji wadogo zilianzishwa kwenye soko ambapo kampuni ya Vodacom kwa kushirikiana na Benki ya CBA wameanzisha huduma ya M-PAWA ambapo wamesajili wakopaji na waweka akiba wadogo wapatao 1,920,712 wenye amana ya shilingi bilioni 18.4. Aidha, kampuni ya Airtel ikishirikiana na taasisi ya huduma ndogo za fedha iitwayo AFB Tanzania Ltd inatoa huduma ya mikopo kwa jina la TIMIZA.

Kutokana na maendeleo hayo, Serikali ilitunga Sheria ya Taifa ya Mifumo ya Malipo ya Mwaka 2015 na kuweka

Kanuni za Fedha za Kielektroniki na Kanuni za Leseni kwa Watoa Huduma wa Mifumo ya Malipo za mwaka 2015 ili kuimarisha usalama, ufanisi na ubunifu wa kielektroniki kwenye huduma ndogo za fedha.

(v) Watoa Huduma za Fedha Wasio Rasmi

Watoa Huduma za fedha wasio rasmi ni pamoja na: Asasi za Kijamii, Vikundi vya kifedha vya kijamii (Ushirika wa Kuweka Akiba na Kukopa kwa Zamu (ROSCAs), Ushirika wa Akiba na Mikopo Vijijini (VSLAs), Ushirika wa Kujiwekea Akiba na Mikopo (ASCAS); Benki za Kijamii za Vijiji (VICOBA); Ushirika wa Akiba na Mikopo, upatu) na wakopeshaji binafsi.

Idadi ya taasisi/vikundi vya fedha visivyo rasmi imeongezeka katika kukidhi mahitaji ya huduma ndogo ya fedha kama mikopo, kuweka akiba na huduma ndogo ya bima. Katika kipindi kilichoishia Machi, 2015 kulikuwa na watoa huduma za fedha wasio rasmi (VICOBA, VSLA, ROSCA) takribani 23,000 wenye wanachama 700,000 na mtaji unaokadiriwa kuwa shilingi bilioni 86. Kwa watumiaji, ujio wa huduma za fedha kwa njia ya simu za kiganjani umepunguza matumizi ya huduma zisizo rasmi kwa nguvu kazi kutoka asilimia 35.1 mwaka 2006 hadi asilimia 6.7 mwaka 2017.

2.2.2 Vikwazo Wakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000

Katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka, 2000 kumekuwepo na vikwazo kama ifuatavyo:-

(i) Upungufu katika Mfumo wa Sheria na Kanuni

Sekta ndogo ya fedha nchini kwa sehemu inasimamiwa na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka, 2006 ambayo imeipa mamlaka Benki Kuu ya Tanzania kutoa leseni, kudhibiti na kusimamia benki na taasisi za fedha (taasisi za huduma ndogo za fedha zinazochukua amana, benki za biashara na benki za wananchi). Aidha, sekta ndogo ya

fedha inaratibiwa na kusimamiwa na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka, 2013 ambayo imeipa Mamlaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kusajili, kudhibiti na kusimamia Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo. Hata hivyo, hakuna taasisi inayohusika na kutoa leseni, kusajili, kudhibiti na kusimamia taasisi ndogo za fedha zisizochukua amana na taasisi za fedha zisizo rasmi.

Upungufu katika mfumo wa sheria na kanuni wakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000, imesababisha utendaji usioridhisha kama: kutokuwepo kwa uwazi kwenye masharti ya ukopeshaji; viwango vya juu vya riba; utoaji holela wa mikopo na wateja kuwa na mikopo mingi inayosababisha limbikizo la madeni; na utaratibu usioridhisha wa ukusanyaji wa madeni. Vile vile, ni vigumu kupata taarifa na takwimu zinazohusiana na uendeshaji wa taasisi ndogo za huduma za fedha zisizosimamiwa.

(ii) Usimamizi Hafifu wa Mifumo ya Taarifa

Taasisi nyingi za huduma ndogo za fedha zisizosimamiwa hazina uwezo wa kukusanya takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusiana na uendeshaji wa shughuli zao pamoja na uwezo mdogo wa uandaaji wa mfumo wa usimamizi wa taarifa. Vilevile, hakuna ufanisi kwenye mfumo wa usimamizi wa taarifa kwenye taasisi ndogo za fedha ikiwa ni pamoja na upungufu kwenye mfumo wa sheria na kanuni ambao umesababisha changamoto kwa Serikali katika ufuatiliaji wa utendaji wa sekta ndogo ya fedha nchini.

(iii) Ukosefu wa Chombo cha Kutunza Taarifa za Mikopo

Uwepo wa taasisi nyingi ndogo za fedha mijini na utoaji wa huduma kwa wateja wale wale pamoja na kukosekana kwa chombo cha pamoja cha ubadilishanaji na uhakiki

wa taarifa za wakopaji umesababisha wakopaji kuwa na mikopo mingi. Tatizo la mikopo mingi limechochewa zaidi na ukosefu wa mfumo sahihi wa utambuzi wa taarifa kamili za wakopaji.

Katika mfumo uliopo wa kurejea taarifa za mikopo, Benki Kuu ya Tanzania imepewa mamlaka ya kukusanya taarifa za wakopaji wa benki na taasisi za fedha ambazo zinaratibiwa na kusimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania. Mfumo huu haujumuiishi wateja wa taasisi ndogo za fedha ambazo hazipo chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Uanzishwaji wa chombo cha kubadilishana taarifa za wakopaji kwa taasisi nyingine za huduma ndogo za fedha utawezesha kuimarika kwa taasisi hizo kwa kupunguza kiwango cha mikopo chechefu na pia kuwasaidia wananchi kuwa na nidhamu ya mikopo ya uhakika na kwa gharama nafuu.

(iv) Mfumo wa Fedha usiwezesha Wananchi wa Kipato cha Chini Kupata Huduma Rasmi za Fedha.

Huduma za fedha nchini zinazotolewa na Benki na Taasisi za huduma ndogo za fedha kwa kiasi kikubwa haziwafikii wananchi kutokana na kutojitosheleza kwa: miundombinu kama nishati, mawasiliano, ulinzi na usalama; matumizi ya hatimiliki za ardhi na mali nyingine, ambazo zinaweza kutumika kama dhamana ili kupata mkopo kutoka taasisi za fedha; elimu na uelewa kuhusu taasisi za fedha na huduma husika; kiwango cha uelewa wa masuala ya fedha; sera na mfumo wa sheria na kanuni hususan katika huduma za taasisi ndogo za fedha.

(v) Kutozingatia sheria ya kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu kutokana na ukosefu wa mamlaka ya usimamizi wa taasisi za huduma ndogo za fedha zisizochukua amana na taasisi za fedha zisizo rasmi.

Sheria ya kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu inawataka wasimamizi wa taasisi za fedha na watoa taarifa wengine

kutekeleza na kuchukua hatua za kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu katika utambuzi na uhakiki wa mteja, ufuatiliaji wa miamala na utunzaji wa kumbukumbu na kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo kwa taasisi wanazozisimamia.

Kutokuwepo kwa mamlaka ya usimamizi wa taasisi za huduma ndogo za fedha zisizochukua amana na taasisi za fedha zisizo rasmi, inakuwa vigumu kubaini taasisi hizo na kufuatilia shughuli zao kwa mujibu wa sheria ya kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu kwa kuwa taasisi hizo hazina leseni, hazisajiliwi, hazidhibitiwi na hazisimamiwi.

2.2.3 Athari Zilizojitokeza wakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000

(i) Kiwango Kikubwa cha Riba

Taasisi za huduma ndogo za fedha nchini zinatoza riba kubwa kwa kuzingatia gharama za mtaji, wafanyakazi, utawala na hasara inayotokana na mikopo. Inakadiriwa kuwa mteja hutozwa hadi theluthi mbili ya riba inayorejeshwa kama gharama za uendeshaji. Hakuna mfumo maalum unaotumiwa na taasisi ndogo za fedha na kampuni kupanga viwango vya riba. Viwango vya riba vinavyotumika vinatofautiana kulingana na aina ya huduma, kiasi cha mkopo, mzunguko na muda wa mkopo. Taasisi nyingi haziko wazi katika mifumo ya upangaji bei na hivyo viwango vya riba huwa vikubwa zaidi ya viwango halisi vya riba vilivyopo na kusababisha wateja kufanya maamuzi ya kukopa bila uelewa wa kutosha. Baadhi ya taasisi ndogo za fedha zinatoza viwango vya juu kuanzia asilimia 3 hadi asilimia 20 kwa kila mwezi.

(ii) Ukosefu wa Utaratibu wa Kuwalinda Watumiaji

Kwa kipindi cha hivi karibuni yamejitokeza malalamiko kutoka kwa umma kuhusiana na mwenendo wa utendaji wa

taasisi ndogo za fedha zinazotoa mikopo ambayo ni: uwepo wa masharti kandamizi kwenye mikataba ya mikopo, utoaji wa mikopo bila kufuata utaratibu, upungufu wa uwazi kwenye masharti ya ukopaji na utaratibu usioridhisha wa ukusanyaji madeni. Mwenendo huu wa biashara unaathiri uzalishaji kwenye kaya na jamii na hivyo kupunguza juhudi za Serikali katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi.

2.2.4 Changamoto Zilizojitokeza katika Kutekeleza Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000

Maendeleo katika sekta ndogo ya fedha yameibua changamoto ambazo ni pamoja na:

(i) Uanzishwaji wa Huduma Mpya na Namna ya Utoaji wa Huduma

Sekta ndogo ya fedha imeleta maendeleo makubwa kwa watoa huduma na huduma zinazotolewa. Maendeleo hayo ni pamoja na kuanzishwa kwa taasisi zisizo za fedha kama vile watoa huduma kwa njia ya mitandao kwa kutumia ubunifu wa teknolojia ili kufikia kaya zenye kipato cha chini. Hata hivyo, maendeleo haya hayakujumuishwa kwenye Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000.

(ii) Ukosefu wa Huduma za Fedha

Pamoja na ongezeko la idadi na aina za benki na taasisi za fedha, upatikanaji wa huduma rasmi za fedha nchini bado ni wa kiwango cha chini. Hii ni kwa mujibu wa takwimu za utafiti wa *FinScope* wa mwaka 2017 ambapo asilimia 28 ya nguvu kazi hawafikiwi na huduma rasmi za fedha. Ukilinganisha takwimu hizo kwa upande wa mijini na vijijini, asilimia 34.9 ni wananchi waishio vijijini na asilimia 14.8 ni wananchi waishio mijini.

(iii) Mitaji Midogo kwenye Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha

Taasisi nyingi za huduma ndogo za fedha zina mitaji

midogo ambayo inatokana na kutokuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba na kutokuwepo kwa vyanzo vya fedha vyenye masharti nafuu na kuaminika. Kwa mfano, SACCOS zinakabiliwa na uwezo mdogo wa kukusanya akiba kutoka kwa wanachama wake ambapo imesababisha kutokuwa na ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya wenye akiba, kufidia hasara za uendeshaji na kutoa mikopo kwa wanachama. Tatizo hili pia limejitokeza kwenye taasisi nyingine za huduma ndogo za fedha.

- (iv) **Uwezo Mdogo wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha**
Taasisi za huduma ndogo za fedha zinakabiliwa na changamoto nyingi zinazofanana kama vile: kuwa na ukomo wa kiutendaji hususan kwenye kuwafikia wananchi na idadi ya wateja wa kuwahudumia; kiwango cha akiba kinachohamasishwa; usimamizi duni wa taarifa za mikopo; uwezo mdogo wa kitaaluma; mfumo hafifu wa utawala bora; Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa usiojitosheleza; uwezo mdogo wa kuandaa hesabu za fedha na utunzaji hafifu wa kumbukumbu; uendeshaji usio na ufanisi; na nidhamu ya fedha.
- (v) **Usimamizi wa Fedha na Programu za Serikali**
Mipango ya Uwezeshaji wananchi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali inakosa uratibu na inatekelezwa na vitengo mbalimbali Serikalini ambapo vingi hukabiliwa na ufinyu wa fedha na kutokuwepo kwa ujuzi stahiki wa usimamizi wa fedha. Mipango hii haijaweza kutengeneza mfumo wa kumuunganisha mwananchi anayekosa huduma za kibenki na taasisi husika. Vilevile, kuna ukosefu wa uhusiano kati ya ongezeko la utoaji mikopo na kuimarisha au kujenga uwezo wa kitaasisi katika ukopeshaji na uendeshaji wenye misingi endelevu.

- (vi) **Ukosefu wa Shirikisho la Taasisi Ndogo za Fedha Kitaifa** Sekta ndogo ya fedha ina shirikisho na mitandao mbalimbali kama vile: Chama cha Taasisi za Kutoa Huduma Ndogo za Fedha Tanzania (TAMFI), Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania, Shirikisho la Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa Tanzania (SCCULT), Dunduliza na Umoja wa SACCOS za wakulima (USAWA). Mitandao mingine ni Shirikisho la Benki za Wananchi Tanzania, Chama cha Benki Tanzania (TBA), Shirikisho la VICOBA Tanzania, Shirikisho la taasisi zisizo rasmi za huduma za fedha Tanzania na Shirikisho la watoa huduma kwa njia ya mtandao . Taasisi hizi huanzishwa kwa hiari na wanachama ambao hawana dira na malengo yanayofanana. Taasisi hizi hutoa huduma pasipo kuwa na chombo cha kuziratibu. Kumekuwepo na changamoto zinazohusiana na mawasiliano, upungufu kwenye mifumo ya udhibiti wa mtandao wa wanachama, kushindwa kuzingatia vigezo, sera na taratibu pamoja na kuvuliwa kwa uanachama pale ambapo wajumbe wa bodi na wafanyakazi kwa maslahi yao badala ya wanachama.

2.3 Umuhimu wa Kufanya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000

Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000 ilijielekeza kuweka msingi imara na wenye ufanisi kwenye mfumo wa taasisi za huduma ndogo za fedha utakao hudumia wananchi wenye kipato cha chini. Sera ilikusudia kufikia malengo kwa: i) Kuanzisha mfumo ambao utawezesha ustawi wa huduma ndogo za fedha; (ii) Kuweka kanuni ambazo zitaelekeza mifumo ya utoaji huduma; (iii) kutoa mwongozo wa kuratibu ushiriki wa kila mhusika katika mfumo; (iv) Kuainisha majukumu ya taasisi na mbinu zitakazotumika ili kusaidia ukuaji wa sekta. Vilevile, utekelezaji wa Sera ulitumia mbinu zifuatazo: (i) udhibiti na usimamizi; (ii) uwekaji na utumiaji wa viwango vya ubora; na (iii) kujenga uwezo.

Katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000 kulijitokeza ongezeko la idadi ya watoa huduma ndogo za fedha ikiwa ni pamoja na benki zinazotoa huduma hizi, taasisi ndogo za fedha, ushiriki wa taasisi zisizo za fedha zinazotumia ubunifu na teknolojia na watoa huduma ndogo za fedha wasio rasmi. Aidha, kumekuwa na mafanikio mengine kama vile kuboreshwa kwa taratibu za utoaji wa huduma. Hata hivyo, utekelezaji wa Sera uliathiriwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mfumo wa sheria na kanuni za kusimamia taasisi zisizochukua amana na taasisi zisizo rasmi, uelewa mdogo wa masuala ya fedha, upungufu wa takwimu katika sekta ya huduma ndogo za fedha, kukosekana kwa mfumo wa kumlinda mtumiaji wa huduma ndogo za fedha, ukosefu wa chombo na utaratibu wa kusuluhisha migogoro, uchache wa aina ya huduma ndogo za fedha na ukosefu wa chombo cha kubadilishana taarifa za mikopo.

Kwa upande mwingine, huduma ndogo za fedha hazijafungamanishwa kikamilifu katika mfumo wa masuala ya fedha pamoja na kuzingatia mabadiliko yatakayolinda sifa ya taasisi hizi. Baadhi ya mahitaji ya kanuni za mfumo wa udhibiti uliopo zinazuia taasisi ndogo za fedha zinazoendeshwa kama asasi zisizo za serikali na kampuni kushindwa kuingia kwenye mfumo wa benki. Aidha, mgawanyiko katika mfumo wa taasisi ndogo za fedha umekwamisha utoaji wa taarifa na ushindani katika sekta hii, ambao umepunguza ufanisi na kuchangia uwepo wa viwango vikubwa vya riba.

Maendeleo mapya na changamoto katika sekta ya huduma ndogo za fedha yamesababisha kufanyika kwa mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000. Aidha, mapitio haya yamechangiwa na ongezeko la hoja mbalimbali kutoka kwa wananchi juu ya uendeshaji wa biashara kwenye taasisi hizi na athari zake katika kupunguza umaskini. Kwa kiasi fulani, hali hii inahusiana na: uwazi mdogo wa vigezo na masharti ya utoaji mikopo; viwango vya juu vya riba; utoaji holela wa mikopo na

wateja kuwa na mikopo mingi inayosababisha limbikizo la madeni; na utaratibu usioridhisha wa ukusanyaji wa madeni.

Mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000 yalilenga kutatua vikwazo, changamoto na masuala yaliyojitokeza katika sekta ndogo ya fedha kwa lengo la kujenga mazingira mazuri ambayo yangechangia maendeleo na uwepo wa ubunifu na huduma stahiki zenye kukidhi mahitaji halisi ya wananchi wa kipato cha chini. Vile vile, Sera mpya inaendana na viwango vya kimataifa baada ya Serikali kuridhia Itifaki za Kikanda na Kimataifa ikiwa ni pamoja na Itifaki ya Umoja wa Kifedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAMU Protocol, 2014*) na Itifaki ya Fedha na Uwekezaji ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC Investment and Finance Protocol, 2014*). Pamoja na mambo mengine, Itifaki hizi zinazitaka nchi wanachama kuoanisha sera zao, sheria na mifumo ya masuala ya fedha ikiwemo sekta huduma ndogo za fedha.

SURA YA TATU

DIRA, DHIMA NA MALENGO

3.1 Dira

Kuwa na sekta ya huduma ndogo za fedha imara, mahiri na jumuishi.

3.2 Dhima

Kuweka mazingira ya sheria na kanuni yanayoweza ukuaji imara wa taasisi za huduma ndogo za fedha zitakazotoa huduma jumuishi za fedha zenye gharama nafuu, ubunifu, endelevu na zinazopatikana kwa urahisi kwa wananchi wenye kipato cha chini, kaya na kampuni za biashara.

3.3 Malengo ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017

3.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la Sera ni kuimarisha huduma jumuishi za kifedha kwa kujenga mazingira wezeshi yatakayoleta ufanisi wa utoaji huduma kwenye sekta ya fedha nchini kwa wananchi wenye kipato cha chini, kaya na shughuli za biashara na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira na kupunguza umaskini.

3.3.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya Sera hii ni:

- (i) Kuhamasisha maendeleo ya sekta ya fedha iliyo imara na jumuishi;
- (ii) Kuwa na uendelevu kwa watoa huduma ndogo za fedha;
- (iii) Kuweka mfumo wa sheria na kanuni ili kuongeza ufanisi kwenye utoaji wa huduma ndogo za fedha;
- (iv) Kukuza utafiti, ubunifu na uendelezaji wa huduma kwenye sekta ndogo ya fedha;
- (v) Kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwenye sekta ndogo ya fedha;
- (vi) Kuhimiza uzingatiaji wa kanuni za utawala bora kwenye sekta ndogo ya fedha; na

- (vii) Kujumuisha masuala ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana katika upatikanaji na utumiaji wa huduma ndogo za fedha zenye usawa na gharama nafuu.

SURA YA NNE

UTEKELEZAJI WA HOJA, MALENGO, MIKAKATI NA SHABAHA YA SERA YA TAIFA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

4.1 Huduma Jumuishi za Fedha

Huduma jumuishi za fedha zina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini pamoja na kuongeza ufanisi wa sera za fedha na utulivu kwenye sekta ya fedha. Uwepo wa huduma za fedha unachangia kukuza ujasiriamali, kupunguza umaskini na kuwapa matumaini ya kupata maendeleo ya kiuchumi. Mwananchi mwenye kipato cha chini, kama mtu mwingine yeyote, anahitaji huduma mbalimbali za fedha kwa ajili ya kuongeza kipato, kuanzisha vitega uchumi na kujihami na majanga. Jitihada mbalimbali zimefanyika kwa lengo la kupanua huduma za fedha nchini kwa wananchi wanaopata huduma hizi kwa kiwango kidogo na wasiopata kabisa. Hii imesababisha kuongezeka kwa idadi na aina ya taasisi za fedha.

Hata hivyo, utendaji wa mfumo wa fedha nchini kama unavyopimwa kwa kuzingatia idadi ya watu na wigo wa upatikanaji wa huduma sio wa kuridhisha ikilinganishwa na viwango vya Afrika. Kiwango cha upatikanaji wa huduma za fedha kwa nguvu kazi ya Taifa kimeongezeka kutoka asilimia 15.9 mwaka 2009 hadi asilimia 65 mwaka 2017. Hii ilitokana na ongezeko la huduma zisizo za benki, hususan uanzishwaji wa huduma za fedha kwa njia ya simu za viganjani. Ulinganisho wa huduma za fedha kati ya mijini na vijijini kwa mwaka 2017, ni asilimia 8.6 tuu ya nguvu kazi ya wananchi waishio vijijini wanaopata huduma za benki ikilinganishwa na asilimia 32.1 ya nguvu kazi kwa wanaoishi mijini. Uwiano wa wananchi waishio vijijini wanaotegemea taasisi zisizo rasmi ulikuwa ni mara tatu ya uwiano wa mijini. Vivyo hivyo, upatikanaji wa huduma za fedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati nchini ni wa kiwango cha chini. Kwa mfano, ni asilimia 20 tu ya wajasiriamali milioni 3.1 nchini walipata huduma za fedha zilizo rasmi kwa mwaka 2010, wakati takriban asilimia 70 hawakutumia huduma yoyote ya fedha.

Pamoja na ongezeko kubwa la idadi na aina ya taasisi ya fedha, upatikanaji wa huduma za fedha zilizo rasmi nchini bado ni wa kiwango cha chini. Hii ilionekana kwenye takwimu za mwaka 2017 ambapo asilimia 28 ya nguvukazi ilikuwa haipati kabisa huduma hizi; asilimia 34.9 ikiwa ni kwa wananchi wa maeneo ya vijijini na asilimia 14.8 ni kwa wananchi wa maeneo ya mijini.

Kiwango kikubwa cha kutokupatikana kwa huduma hizi nchini kwa sehemu kinachangiwa na benki na taasisi za huduma ndogo za fedha kutofika maeneo mengi kutokana na miundombinu isiyotosheleza, kipato kidogo na kisicho cha uhakika kinachotokana na utegemezi kwenye shughuli za kilimo zenye tija ndogo na za msimu na ukosefu wa ajira; Ukosefu wa hatimiliki za ardhi na mali nyingine ambazo zingeweza kutumika kama dhamana ya mikopo kwenye taasisi za fedha; uelewa mdogo kuhusu taasisi za fedha na huduma zinazotolewa; elimu ndogo ya masuala ya fedha; kutokuwepo kwa huduma zinazokidhi mahitaji ya watumiaji; kutokuwa na ubunifu na uwezo mdogo wa kiutendaji kwa watoa huduma; na viwango vikubwa vya riba.

Lengo: Kuhamasisha maendeleo ya sekta ya fedha iliyo imara na jumuiishi.

Mikakati

- (i) Kuhamasisha Sekta za umma na binafsi kuwekeza katika miundombinu ambayo inasaidia maendeleo ya sekta ndogo ya fedha;
- (ii) Kupanua wigo wa Serikali katika kusaidia maendeleo ya biashara ndogo na za kati;
- (iii) Kuhamasisha upatikanaji wa fedha/mitaji kwenye mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo;
- (iv) Kuimarisha taratibu za usajili wa hatimiliki za ardhi na mali;
- (v) Kuhamasisha utoaji wa mikopo midogo ya muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba katika maeneo ya vijijini;
- (vi) Kuhimiza taasisi za watoa huduma ndogo za fedha kutoa huduma maeneo ya vijijini;
- (vii) Kuhimiza huduma ya kuendeleza biashara katika sekta ndogo ya fedha; na

(viii) Utoaji wa elimu ya fedha na ufahamu juu ya huduma ndogo za fedha nchini.

Shabaha

- (i) Programu za kuwajengea uwezo watoa huduma ndogo za fedha juu ya matumizi ya teknolojia inayojumuisha Usimamizi wa Mifumo ya Habari (MIS) na kampuni za simu za kiganjani katika sekta ndogo ya fedha zitakuwa zimetekelezwa ifikapo mwaka 2018;
- (ii) Kuoanisha na kupitia sheria zitakazosaidia ubunifu katika teknolojia ya habari na mawasiliano ifikapo mwaka 2028;
- (iii) Miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) katika sekta ndogo ya fedha kuongezeka ifikapo mwaka 2028;
- (iv) Tafiti juu ya tathmini ya Mifuko na programu za Serikali inayosaidia biashara ndogo na za kati kufanyika ifikapo Juni 2018;
- (v) Kuanzisha na kuimarisha vituo vya kuendeleza biashara ndogo na za kati ifikapo mwaka 2020;
- (vi) Kuiongezea mtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ili iweze kukopesha na kusaidia wakulima wadogo ifikapo Juni, 2028;
- (vii) Utafiti juu ya tathmini ya matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani kama dhamana mbadala kufanyika ifikapo mwaka 2019;
- (viii) Elimu kwa umma juu ya Soko la Bidhaa kufanyika ifikapo mwaka 2018;
- (ix) Kuongeza kasi ya upimaji, usajili na utoaji wa hatimiliki za ardhi nchini kote ifikapo Juni 2028;
- (x) Programu za kujenga uwezo kuhusu mikopo midogo ya ujenzi wa nyumba kufanyika ifikapo Juni, 2028;
- (xi) Elimu kwa umma juu ya Mfuko wa Mikopo Midogo ya Ujenzi wa Nyumba kufanyika ifikapo mwaka 2019;
- (xii) Uwezo wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na taasisi za fedha zilizopo maeneo ya vijijini katika kutoa huduma za fedha maeneo ya vijijini kujengwa ifikapo mwaka 2028;
- (xiii) Utaratibu wa mpango wa dhamana ya mikopo ya kilimo kwa maeneo ya vijijini kuanzishwa ifikapo mwaka 2028;
- (xiv) Mfumo wa usimamizi wa watoa huduma za kuendeleza biashara kuanzishwa ifikapo mwaka 2019;
- (xv) Mazingira mazuri ya mafunzo kupitia ushiriki wa biashara na maonyesho kuwekwa ifikapo mwaka 2028;

- (xvi) Mwongozo wa mafunzo kwa ajili ya watoa huduma za maendeleo ya Biashara kuandaliwa ifikapo mwaka 2019;
- (xvii) Miongozo ya elimu ya fedha katika sekta ndogo ya fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2019;
- (xviii) Mpango wa elimu ya huduma ndogo za fedha kwa ajili ya umma kuwepo ifikapo mwaka 2019;
- (xix) Warsha ya wadau ya kujadili elimu ya fedha kufanyika ifikapo mwaka 2019; na
- (xx) Elimu kwa umma juu ya huduma ndogo za fedha kutolewa ifikapo mwaka 2028.

4.2 Uendelevu wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha

Uendelevu wa taasisi za huduma ndogo za fedha ni muhimu katika utoaji wa huduma maeneo ya mijini na vijijini. Uwezo wa watoa huduma ndogo za fedha ni msingi wa ukuaji endelevu na kuenea kwa taasisi ndogo za fedha. Kwa sasa, watoa huduma ndogo za fedha walio wengi nchini hutegemea mitaji na uwezo wa kujiendesha kutoka benki za biashara, mifuko ya hifadhi za jamii, washirika wa maendeleo, programu za Serikali za uwezeshaji wananchi na wawekezaji wengine kutoka nje ya nchi.

Hata hivyo, taasisi nyingi za huduma ndogo za fedha zina changamoto zinazofanana ikiwa ni pamoja na ukosefu wa ukwasi wa kutosha na ongezeko la mitaji, utegemezi mkubwa wa fedha kutoka vyanzo vya nje, uratibu usioridhisha wa programu za Serikali za uwezeshaji wananchi kiuchumi, uhaba wa wafanyakazi wenye ujuzi, utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha, uwezo mdogo wa kitaasisi, mitaji midogo, utamaduni mdogo wa uwekaji akiba, usimamizi mdogo wa urejeshaji madeni na kutokuwa na uwezo wa kuhudumia mkopaji mmoja mmoja.

Lengo: Kuwa na uendelevu kwa watoa huduma ndogo za fedha.

Mikakati:

- (i) Kuhimiza watoa mikopo ya jumla watoe mikopo ya gharama nafuu kwa watoa huduma ndogo za fedha;
- (ii) Kukuza utamaduni wa kuweka akiba miongoni mwa wananchi wa kipato cha chini;
- (iii) Kujenga uwezo kwa watoa huduma ndogo za fedha;
- (iv) Kuhamasisha utumiaji wa teknolojia ya habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika sekta ndogo ya fedha;
- (v) Kuhamasisha mabadiliko ya watoa huduma ndogo za fedha kupanda daraja moja kwenda daraja nyingine;
- (vi) Kuimarisha uratibu wa Serikali katika Mifuko na programu za huduma ndogo za fedha;
- (vii) Kuweka utaratibu wa kuunganisha taasisi za fedha zisizo rasmi na watoa huduma rasmi za fedha; na
- (viii) Kuanzishwa kwa utaratibu wa kupima utendaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha.

Shabaha:

- (i) Kanuni za watoa mikopo ya jumla katika sekta ndogo ya fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2019;
- (ii) Utaratibu kwa taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha kushiriki katika soko la mitaji uwe umeandaliwa ifikapo mwaka 2019;
- (iii) Programu ya kuwaelimisha wananchi wa kipato cha chini manufaa ya kuweka akiba kufanyika ifikapo Juni, 2020;
- (iv) Programu ya elimu ya fedha kuingizwa kwenye mitaala ya shule na vyuo vikuu ifikapo Juni, 2020;
- (v) Mfumo wa kuwajengea uwezo watoa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Juni, 2019;
- (vi) Mwongozo wa mafunzo kwa watoa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Juni, 2019;
- (vii) Programu za mafunzo kwa watoa huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo mwaka 2019;
- (viii) Mkutano mkuu wa kila mwaka kwa wadau wa taasisi za huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo mwaka 2019;

- (ix) Mfuko wa kugharamia kujenga uwezo uwe umejumuishwa ndani ya mfumo wa usimamizi wa huduma ndogo za fedha ifikapo Juni, 2020;
- (x) Programu ya elimu kuhusu huduma ndogo za fedha kwa njia ya elekitroniki iwe imefanyika ifikapo Juni 2019;
- (xi) Mfumo wa kanuni za utoaji wa huduma ndogo za fedha kwa njia ya elekitroniki kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini kuanzishwa ifikapo Juni, 2019;
- (xii) Kanuni zitakazotoa mwongozo wa kutoka daraja moja kwenda daraja lingine kwa watoa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Desemba, 2019;
- (xiii) Tathmini ya Mifuko na Programu za Serikali kuhakikisha uendelevu kufanyika ifikapo Juni, 2028;
- (xiv) Mifumo ya sheria na kanuni za mifuko na programu za Serikali kuoanishwa ifikapo Juni, 2019;
- (xv) Mifumo ya uendeshaji ya Mifuko na Programu za Serikali kuoanishwa ifikapo Juni, 2019;
- (xvi) Mwongozo wa uendeshaji kwa vikundi vya kifedha vya kijamii kuandaliwa ifikapo mwaka 2020;
- (xvii) Kanuni za maadili kwa vikundi vya kifedha vya kijamii kuandaliwa ifikapo mwaka 2020;
- (xviii) Kuviunganisha vikundi vya kifedha vya kijamii na watoa huduma za fedha rasmi ifikapo Juni, 2019
- (xix) Mwongozo wa kupima utendaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2019; na
- (xx) Mafunzo kwa taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha na elimu kwa umma kuhusu upimaji wa utendaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo mwaka 2028.

4.3 Usimamizi wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha

Kanuni na usimamizi wa taasisi za huduma ndogo za fedha zinapaswa kuwa sehemu muhimu ya mkakati wa kuendeleza sekta ndogo ya fedha kwa misingi ya soko. Huduma ndogo za fedha zinajumuisha mikopo, akiba, bima ndogo na uhaulishaji wa fedha. Maendeleo hayo yalichochea ubunifu katika kufanikisha huduma endelevu za fedha zinazohitaji mfumo wa sheria kwa ajili ya udhibiti na usimamizi. Udhibiti na

usimamizi wa taasisi za huduma ndogo za fedha utasaidia kumlinda mtumiaji wa huduma hizo.

Hivi sasa, kuna kasi ya ukuaji na ongezeko la wadau mbalimbali katika sekta ndogo ya fedha, ikiwa ni pamoja na kampuni na asasi zisizo za serikali za huduma ndogo za fedha za ndani na za kigeni zinazohamasisha sekta ndogo ya fedha zisizo na udhibiti na usimamizi. Utendaji wao umesababisha malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusiana na kumlinda mtumiaji wa huduma ikiwa ni pamoja na: kuwa na masharti kandamizi kwenye mikataba ya mikopo, utoaji holela wa mikopo, usimamizi mbaya wa akiba, upungufu wa uwazi kwenye masharti ya ukopaji, kutokuwa na usiri, kutokuwa na utaratibu wa utatuzi wa malalamiko, utaratibu usioridhisha wa ukusanyaji madeni na viwango vikubwa vya riba.

Lengo: Kuweka mfumo wa sheria na kanuni ili kuongeza ufanisi kwenye utoaji wa huduma ndogo za fedha

Mikakati:

- (i) Kutungwa kwa sheria ya huduma ndogo za fedha;
- (ii) Kuweka mkazo kwa watoa huduma ndogo za fedha kuzingatia kanuni za kuwalinda watumiaji wa huduma ndogo za fedha; na
- (iii) Kuweka mfumo wa sheria wa kubadilishana taarifa katika sekta ndogo ya fedha.

Shabaha:

- (i) Sheria ya huduma ndogo za fedha kutungwa ifikapo mwaka 2019;
- (ii) Kanuni za huduma ndogo za fedha kutungwa ifikapo mwaka 2019;
- (iii) Mwongozo wa uendeshaji kwa watoa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Oktoba, 2019;
- (iv) Elimu kwa umma kuhusu mfumo wa sheria na kanuni za huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo Novemba, 2019;
- (v) Sheria na Kanuni za huduma ndogo za fedha kutolewa kwa umma ifikapo Desemba, 2019;
- (vi) Kanuni za kumlinda mtumiaji wa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Juni, 2019;
- (vii) Mwongozo wa kumlinda mtumiaji wa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Juni, 2019;

- (viii) Kanzidata ya sekta ya fedha kuanzishwa ifikapo Juni, 2019;
- (ix) Kanuni kwa watoa huduma ndogo za fedha kutoa taarifa za wateja kwenye chombo cha kutunza taarifa za mikopo kuwekwa ifikapo Juni, 2019;
- (x) Elimu kwa umma juu ya matumizi bora ya chombo cha kutunza taarifa za mikopo kutolewa ifikapo Septemba, 2019; na
- (xi) Mfumo wa sheria na kanuni wa kubadilishana taarifa kati ya wasimamizi wa sekta ndogo ya fedha kuwekwa ifikapo Juni, 2019.

4.4 Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Huduma za Sekta Ndogo ya Fedha

Serikali inatambua kuwa utafiti, ubunifu na uendelezaji wa huduma za sekta ya huduma ndogo ya fedha ni muhimu katika ukuaji, ueneaji na uendelevu wa sekta hiyo. Shughuli zinazoendelea za utafiti, ubunifu na uendelezaji wa huduma ndogo za fedha ni sehemu muhimu ya mfumo wa soko kwa maendeleo ya sekta ya huduma ndogo ya fedha. Taarifa mpya kuhusu huduma ndogo za fedha zinahitajika wakati wote kwenye sekta ili kuelekeza, kuhamasisha na kutoa uelewa kwa lengo la kusaidia wadau, kuongeza wigo wa huduma pamoja na kuweka misingi ya ufuatiliaji na tathmini.

Wadau kadhaa kwenye sekta ndogo ya fedha zikiwemo taasisi za elimu na taasisi ndogo za huduma za fedha wameendelea kufanya utafiti, ubunifu na kuendeleza huduma ndogo za fedha ingawa matokeo yaliyopatikana hayatumwiwi na sekta hiyo. Hali hii imechangiwa na uwepo wa takwimu zisizo za uhakika, kutofautiana kwa taarifa, uhaba wa rasilimali na uwezo mdogo wa utendaji. Hivyo, kuna umuhimu wa kutatua hali hiyo ili kuwa na sekta mahiri inayojielekeza kwenye mahitaji halisi ya wananchi wa kipato cha chini.

Lengo: Kuongeza utafiti, ubunifu na uendelezaji wa huduma katika sekta ya huduma ndogo ya fedha.

Mikakati:

- (i) Kuongeza uwezo wa watunga sera na wadau wa sekta ya huduma ndogo ya fedha kufanya tafiti;
- (ii) Kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kufanya tafiti;

- (iii) Kuhamasisha ubunifu wa huduma ndogo za fedha; na
- (iv) Kuboresha uenezaji na ubadilishanaji wa taarifa za matokeo ya utafiti kwa umma.

Shabaha:

- (1) Programu za kujenga uwezo kwa watunga sera, wanataaluma, na wadau wengine katika huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2028;
- (2) Utafiti wa kukuza sekta ndogo ya fedha kufanyika ifikapo mwaka 2028;
- (3) Watafiti wa ndani kushiriki katika tafiti za kikanda na kimataifa za huduma ndogo za fedha ifikapo mwaka 2028;
- (4) Mifuko ya ubunifu katika sekta ndogo ya fedha kuimarishwa ifikapo Juni, 2028;
- (5) Shindano la mwaka la ubunifu wa huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo Juni, 2028; na
- (6) Matokeo ya utafiti kutolewa kwa umma ifikapo mwaka 2028.

4.5 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

Ushirikiano na jumuiya za kikanda na kimataifa ni muhimu katika maendeleo ya sekta ndogo ya fedha. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa jumuiya za kikanda na kimataifa ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Ushirikiano wa Maendeleo wa Nchi za Kusini mwa Afrika na mtandao wa kimataifa wa huduma ndogo za fedha. Kuna itifaki mbalimbali katika masuala yanayohusu huduma ndogo za fedha ambazo zimesainiwa na kuridhiwa na Serikali. Pamoja na mambo mengine, itifaki hizo zinazitaka nchi wanachama kuoanisha sera, sheria na mifumo ya fedha ikijumuisha sekta ndogo ya fedha. Hivyo, kuna umuhimu wa kuimarisha ushirikiano na jumuiya za kimataifa ili kufaidika na huduma mbalimbali, rasilimali na uzoefu.

Lengo: Kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwenye sekta ndogo ya fedha.

Mikakati:

- (i) Kuoanisha mfumo wa sera, sheria na kanuni kwa masuala ya huduma ndogo za fedha ya kulingana na ushirikiano wa kikanda na kimataifa;
- (ii) Kutangaza fusra za uwekezaji zilizopo katika sekta ya huduma ndogo ya fedha kwa jumuiya za kikanda na kimataifa; na
- (iii) Kuanzisha mtandao wa usimamizi kikanda kwa lengo la kusimamia udhibiti wa majanga na utatuzi wa migogoro.

Shabaha:

- (i) Tathmini katika sekta ndogo ya fedha kwa kuzingatia mikataba na itifaki za kikanda na kimataifa kufanyika ifikapo mwaka 2020;
- (ii) Mifumo ya sheria na kanuni kwenye sekta ndogo ya fedha kuoanishwa na viwango vya kikanda na kimataifa ifikapo mwaka 2020;
- (iii) Itifaki na makubaliano yanayohusiana na sekta ndogo ya fedha kuridhiwa ifikapo mwaka 2028;
- (iv) Kushiriki kwenye mikutano ya kikanda na kimataifa ifikapo mwaka 2028;
- (v) Mipango ya uelewa juu ya fursa zilizopo za uwekezaji kikanda na kimataifa kufanyika ifikapo mwaka 2028;
- (vi) Mikataba ya uwekezaji baina ya nchi wanachama na mashirika ya kimataifa kuhusu sekta ndogo ya fedha kujadiliwa ifikapo mwaka 2020;
- (vii) Miongozo ya ushirikiano mipakani kwa wasimamizi wa sekta ndogo ya fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2020;
- (viii) Mikataba ya makubaliano baina ya mamlaka za usimamizi wa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2019; na
- (ix) Programu za uhamasishaji kwa ajili ya kuoanisha taratibu za mipaka na mamlaka nyingine za usimamizi kwa lengo la kuzingatia kanuni na viwango vya soko kufanyika ifikapo mwaka 2019.

4.6 Utawala Bora katika Sekta Ndogo ya Huduma za Fedha

Mafanikio ya utoaji wa huduma za fedha kwa kiasi kikubwa yanategemea utawala bora kwenye taasisi za huduma ndogo za fedha katika kutoa huduma stahili ili kuwa na sekta mahiri. Uwepo wa uangalizi na

usimamizi wa nje ni muhimu kwa ustawi wa sekta. Hata hivyo, uangalizi wa nje hauwezi kuchukua nafasi ya uwajibikaji unaotokana na utawala na usimamizi sahihi unaofanywa na wamiliki na wakurugenzi wa taasisi za fedha.

Viwango, mahitaji ya utoaji taarifa na kanuni za maadili kwenye shirikisho la watoa huduma ndogo za fedha ni njia ya kawaida ya kuongeza uwazi. Matakwa ya viwango vya uhasibu na ukaguzi kutoka nje yanasaidia kuhimiza taasisi ndogo za fedha kutoa taarifa sahihi za hesabu, taarifa za fedha zenye uwazi na zinazojitosheleza, na mifumo ya uendeshaji na usimamizi iliyoboreshwa. Utoaji wa taarifa (na utoaji wa taarifa kwa hiari unaozingatia viwango vya ubora) unaongeza uwazi na pia ni motisha ya kuboresha utendaji, hususan pale ambapo vigezo vinatumika. Miaka kadhaa iliyopita, imeonesha kwamba taasisi za huduma ndogo za fedha zimekuwa na utawala usioridhisha, usimamizi dhaifu wa mikopo na urejeshaji madeni, utaratibu usioridhisha wa kupanga gharama za huduma na uwezo mdogo wa usimamizi. Kukosekana kwa utawala sahihi kwa taasisi kunaongeza athari za usimamizi na kunaondoa imani kwa wananchi juu ya taasisi za huduma ndogo za fedha.

Lengo: Kuhimiza uzingatiaji wa kanuni za utawala bora kwenye sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha.

Mikakati:

- (i) Kuimarisha uwajibikaji, usawa na uwazi kwa wadau wote wa sekta ndogo ya fedha; na
- (ii) Kuweka mfumo wa sheria na kanuni kwa taasisi za huduma ndogo za fedha kutoa taarifa za vyanzo vya fedha kwa mujibu wa sheria ya kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu.

Shabaha:

- (i) Miongozo kuhusu utawala bora kwenye sekta ndogo ya fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2019;
- (ii) Taasisi za huduma ndogo za fedha katika kuzingatia miongozo ya utawala bora kwenye sekta ya huduma ndogo za fedha kufuatiliwa ifikapo mwaka 2028;

- (iii) Mfumo wa Sheria na kanuni kwa taasisi za huduma ndogo za fedha kutoa taarifa za vyanzo vya fedha kwa mujibu wa sheria ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu kuwekwa ifikapo 2028; na
- (iv) Elimu kuhusiana na udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu kwenye sekta ndogo ya fedha kutolewa ifikapo mwaka 2028.

4.7 Makundi yenye Mahitaji Maalum, Jinsia na Vijana

Sekta ndogo ya fedha ina uwezo wa kusaidia makundi yenye mahitaji maalum, wanawake na vijana kuwawezesha kiuchumi. Kuimarisha makundi hayo kwa fedha kutayawezesha kuchangia kiuchumi kwenye familia na jamii zao ambako kutaleta matokeo chanya kiuchumi, na hivyo kuongeza ujasiri na uhakika wa maisha yao. Pamoja na mchango unaotolewa na makundi haya nchini, wengi wao hawajafikiwa na huduma ndogo za fedha. Kutokana na utafiti wa *FinScope* wa mwaka 2017, asilimia 30.3 ya wanawake wenye uwezo wa kufanya kazi walikuwa hawajafikiwa na huduma za fedha ikilinganishwa na asilimia 25.5 ya wanaume wenye uwezo wa kufanya kazi. Aidha, idadi ya SACCOS imeongezeka kwa kiasi kikubwa, ambapo asilimia 60 ya wanachama ni wanaume. Vile vile, wanawake wanakabiliwa na changamoto ya mila na desturi ambazo haziharuhusu kumiliki baadhi ya mali ambazo zinaweza kutumika kama dhamana. Ingawa hakuna taarifa za kutosha juu ya vijana kupata huduma za fedha lakini inaonesha kuwa wengi wao pia hawajafikiwa na huduma za fedha.

Lengo: Kujumuisha masuala ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana katika upatikanaji na utumiaji wa huduma ndogo za fedha zenye usawa na kwa gharama nafuu.

Mikakati:

- (i) Kutoa elimu kwa makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kuhusu huduma ndogo za fedha zilizopo; na
- (ii) Kuhamasisha watoa huduma ndogo za fedha kuendeleza ubunifu kwenye utoaji wa huduma ili kukidhi mahitaji ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana.

Shabaha:

- (i) Programu za uhamasishaji wa makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana katika sekta ndogo ya fedha kutekelezwa ifikapo mwaka 2028;
- (ii) Mafunzo ya ujasiriamali kwa makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kufanyika ifikapo mwaka 2028;
- (iii) Makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kuhamasishwa kuunda makundi ya huduma za fedha ifikapo mwaka 2028;
- (iv) Huduma ndogo za fedha zinazokidhi mahitaji ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kutolewa ifikapo Juni, 2020; na
- (v) Mfumo wa utoaji taarifa kwa kila kundi lenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kutoka kwa taasisi za huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Juni, 2020.

SURA TANO

BANGO KITITA LA MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA YA MWAKA, 2017

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
1. Kuhamasisha maendeleo ya sekta ya fedha iliyo imara na jumuishi.	(i) Kuhamasisha sekta za umma na binafsi kuwekeza katika miundombinu ambayo inasaidia maendeleo ya sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha.	(i) Programu za kuwajengea uwezo watoa huduma ndogo za fedha juu ya matumizi ya teknolojia inayojumuisha Usimamizi wa mifumo ya habari (MIS) na kampuni za simu za kiganjani katika sekta ndogo ya fedha zitakuwa zimetekelezwa ifikapo mwaka 2019;	750,000	Juni, 2019	PMO, MOFP, BOT, TPSE, TCRA, Watoa Huduma za Mifumo ya Malipo
		(ii) Kuoanisha na kupitia sheria zitakazosaidia ubunifu katika teknolojia ya habari na mawasiliano ifikapo mwaka 2028;	600,000	Juni, 2028	PMO, MOFP, BOT, TPSE, TCRA, Watoa Huduma za Mifumo ya Malipo

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
		(iii) Miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) katika sekta ndogo ya fedha kuongezeka ifikapo mwaka 2028;	240,000	Juni, 2028	PMO, MOFP, TIC, BOT, TPSE, TCRA, Watoa Huduma za Mifumo ya Malipo, MFIs
	(ii) Kupanua wigo wa Serikali katika kusaidia maendeleo ya biashara ndogo na za kati.	(i) Tafiti juu ya tathmini ya Mifuko na programu za Serikali inayosaidia biashara ndogo na za kati kufanyika ifikapo Juni 2019;	1,500,000	Juni, 2019	PMO, MOFP, MITI, NEEC,

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(iii) Kuhamasisha upatikanaji wa fedha/ mitaji kwenye mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo.	(i) Kuiongeza mtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ili iweze kukopesha na kusaidia wakulima wadogo ifikapo Juni 2028; (ii) Utafiti juu ya tathmini ya matumizi ya mfumo wa stakbadhi ghalani kama dhamana mbadala kufanyika ifikapo mwaka 2019;	900,000,000	Juni, 2028	MOFP, BOT, MALF
	(iv) Kuimarisha taratibu za usajili wa hatimiliki za ardhi na mali.	(iii) Elimu kwa umma juu ya Soko la Bidhaa kufanyika ifikapo mwaka 2019; (i) Kuiongeza kasi ya upimaji, usajili na utoaji wa hatimiliki za ardhi nchini kote ifikapo Juni 2028;	1,150,000	Juni, 2019	MOFP, MALS, MITI MOFP, CMSA, Tanzania Mercantile Exchange
			1,400,000	Juni, 2028	MLHHS, LGAs, MKURABITA,

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(v) Kuhamasisha utoaji wa mikopo midogo ya muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba katika maeneo ya vijijini.	(i) Programu za kujenga uwezo kuhusu mikopo midogo ya ujenzi wa nyumba kufanyika ifikapo Juni, 2028;	300,000	Juni, 2028	MOFP, MLHHS, LGAs, BOT, MFIs
		(ii) Elimu kwa umma juu ya Mfuko wa Mikopo Midogo ya Ujenzi wa Nyumba kufanyika ifikapo mwaka 2019;	960,000	Juni, 2019	MOFP, MLHHS, LGAs, MFIs
	(vi) Kuhimiza taasisi za watoa huduma ndogo za fedha kutoa huduma maeneo ya vijijini.	(i) Uwezo wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na taasisi za fedha zilizopo maeneo ya vijijini katika kutoa huduma za fedha maeneo ya vijijini kujengwa ifikapo mwaka 2028;	600,000	Juni, 2028	MOFP, TADB, MFIs, MIVARF/PMO, FSDT
		(ii) Utaratibu wa mpango wa dhamana ya mikopo ya kilimo kwa maeneo ya vijijini kuanzishwa ifikapo mwaka 2028;	150,000	Juni, 2028	MOFP, TADB, BOT

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(vii) Kuhimiza huduma ya kuendeleza biashara katika sekta ndogo ya fedha.	(i) Mfumo wa Usimamizi wa watoa huduma ya kuendeleza biashara kuanzishwa ifikapo mwaka 2019;	300,000	Juni, 2019	MOFP, BOT, TCDC, TAMFI, LGAs, BDS
		(ii) Mazingira mazuri ya mafunzo kupitia ushiriki wa biashara na maonyesho kuwekwa ifikapo mwaka 2028;	300,000	Juni, 2028	MOFP, MITI, LGAs, MKURABITA
		(iii) Mwongozo wa mafunzo kwa ajili ya watoa huduma ya kuendeleza Biashara kuandaliwa ifikapo mwaka 2019;	300,000	Juni, 2019	MOFP, BOT, TAMFI, BDS

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(viii) Utoaji wa elimu ya fedha na ufahamu juu ya huduma ndogo za fedha nchini.	(i) Miongozo ya elimu ya fedha katika sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2019;	150,000	Juni, 2019	MOFP, TCDC BOT, TAMFI, LGAs,
		(ii) Mpango wa elimu ya fedha kwa ajili ya umma kuwepo ifikapo mwaka 2019;	300,000	Juni, 2019	MOFP, TCDC BOT, TAMFI, LGAs,
		(iii) Warsha ya wadau ya kujadili elimu ya fedha kufanyika ifikapo mwaka 2019; na	150,000	Juni, 2019	MOFP, BOT
		(iv) Elimu kwa umma juu ya huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo mwaka 2028	1,800,000	Juni, 2028	MOFP, TCDC BOT, TAMFI, LGAs,

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
2. Kuwa na uendelevu kwa watoa huduma ndogo za fedha.	(i) Kuhimiza watoa mikopo ya jumla watoe mikopo ya gharama nafuu kwa watoa huduma ndogo za fedha.	(i) Kanuni za watoa mikopo ya jumla katika sekta ndogo ya fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2019; (ii) Utaratibu kwa taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha kushiriki katika soko la mitaji uwe umeandaliwa ifikapo mwaka 2019;	150,000	Juni, 2019	MOFP, BOT, TCDC, LGA,s, SSRA
			600,000	Juni, 2019	MOFP, CMSA, TAMFI

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(ii) Kukuza utamaduni wa kuweka akiba miongoni mwa wananchi wa kipato cha chini.	(i) Programu ya kuwaelimisha wananchi wa kipato cha chini manufaa ya kuweka akiba kufanyika ifikapo Juni, 2020;	900,000	Juni, 2020	MOFP, BOT, TCDC, LGA's
		(ii) Programu ya elimu ya fedha kuingizwa kwenye mitaala ya shule na vyyuo vikuu ifikapo Juni, 2020;	200,000	Juni, 2020	MOFP, BOT, CMSA, TCDC, TPSE, Pension Funds, MFIs
		(iii) Mfumo wa kuwajengea uwezo watoa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Juni, 2020;	300,000	Juni, 2020	MOFP, MoEVT BOT, TCDC,

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(iii) Kujenga uwezo kwa watoa huduma ndogo za fedha.	(i) Muundo wa mafunzo kwa watoa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo mwaka, 2028;	300,000	Juni, 2028	MOFP, TCDC BOT, TAMFI, LGAs,
		(ii) Mwongozo wa mafunzo kwa watoa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo mwaka, 2028;	300,000	Juni, 2028	MOFP, TCDC BOT, TAMFI, LGAs,
		(iii) Programu za mafunzo kwa watoa huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo mwaka 2028;	300,000	Juni, 2028	MOFP, BDS, BOT, TCDC, TAMFI
		(iv) Mkutano Mkuu wa kila mwaka kwa wadau wa taasisi za huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo mwaka 2028;	1,200,000	Septemba, 2028	MOFP, BDS, BOT, TCDC, LGAs, NEEC TAMFI
		(v) Mfuko wa kugharamia kujenga uwezo uwe umejumuishwa ndani ya mfumo wa usimamizi wa huduma ndogo za fedha ifikapo Juni, 2020;	1,200,000	Juni, 2020	MOFP, TCDC, LGAs, BOT, MIVARF/PMO, FSDT, MFIs, NEEC and Development Partners

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(iv) Kuhamasisha utumiaji wa teknolojia ya habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika sekta ndogo ya fedha.	(i) Programu ya elimu kuhusu huduma ndogo za fedha kwa njia ya digitali iwe imefanyika ifikapo Juni 2019; (ii) Mfumo wa kanuni za utoaji wa huduma ndogo za fedha kwa njia ya digitali kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini kuanzishwa ifikapo Juni, 2019;		Juni, 2019	MOFP, LGAs, BOT, TCRA, MIVARF/PMO, FSĐT, MFIs
	(v) Kuhamasisha mabadiliko ya watoa huduma ndogo za fedha kupanda daraja moja kwenda daraja nyingine.	(i) Kanuni zitakazotoa mwongozo wa kutoka daraja moja kwenda daraja lingine kwa watoa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Desemba, 2019;	200,000	Desemba, 2019	MOFP, BOT, AGC, MITI, BRELA, TCDC, LGAs, MFIs

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(vi) Kuimarisha uratibu wa Serikali katika Mifuko na programu za huduma ndogo za fedha.	(i) Tathmini ya Mifuko na Programu za za Serikali kuhakikisha uendelevu kufanyika ifikapo Juni, 2028 (ii) Mifumo ya sheria na kanuni za mifuko na programu za Serikali kuoanishwa ifikapo Juni, 2019; (iii) Mifumo ya uendesaji ya Mifuko na Programu za Serikali kuoanishwa ifikapo Juni, 2019;	300,000	Juni, 2028	NEEC, PMO, MOE, BOT, TCDC, MITI, SIDO, MIVARF/ PMO, FSDI, PO-TAMISEMI,
			150,000	Juni, 2019	MHCDGSC, MAFC, , MNRT, , MITI, MLHHS,
			150,000	Juni, 2019	MKURABITA, LGAs, MFIs, MSMEs

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(vii) Kuweka utaratibu wa kuunganisha vikundi vya kifedha vya kijamii na watoa huduma rasmi za fedha.	(i) Mwongozo wa uendeshaji kwa vikundi vya kifedha vya kijamii kuandaliwa ifikapo mwaka 2020; (ii) Kanuni za maadili kwa vikundi vya kifedha vya kijamii kuandaliwa ifikapo mwaka 2020; (iii) Kuvijumuisha vikundi vya kifedha vya kijamii na watoa huduma za fedha rasmi ifikapo Juni, 2020	150,000	Juni, 2020	MOFP, BOT, TCDC, LGAs, FSĐT, MIVARF, TAMFI.
			300,000	Juni, 2020	MOFP, LGA's
			750,000	Juni, 2020	MOFP, TCDC, LGAs, BOT, MIVARF/PMO, FSĐT, TAMFI

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(viii) Kuanzishwa kwa utaratibu wa kupima utendaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha.	(i) Mwongozo wa kupima utendaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2019;	300,000	Juni, 2019	MOFP, TCDC, LGAs, BOT, MIVARF/PMO, FSĐT, TAMFI
		(ii) Mafunzo kwa taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha na elimu kwa umma kuhusu upimaji wa utendaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo mwaka 2028.	300,000	Juni, 2028	MOFP, TCDC, LGAs, BOT, MIVARF/PMO, FSĐT, TAMFI

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
3. Kuweka mfumo wa sheria na kanuni ili kuongeza ufanisi kwenye utoaji wa huduma ndogo za fedha	(i) Kutungwa kwa sheria ya huduma ndogo za fedha.	(i) Sheria ya huduma ndogo za fedha kutungwa ifikapo mwaka 2018;	500,000	Desemba, 2018	MOFP, BOT, AGC, TCRA, TCDC, LGA's, MFIs
		(ii) Kanuni za huduma ndogo za fedha kutungwa ifikapo mwaka 2019;	300,000	Desemba, 2019	MOFP, BOT, AGC, TCRA, TCDC, LGA's, MFIs
		(iii) Mwongozo wa uendeshaji kwa watoa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Oktoba, 2019;	150,000	Oktoba, 2019	MOFP, BOT, AGC, TCRA, TCDC, LGA's, MFIs
		(iv) Elimu kwa umma kuhusu mfumo wa sheria na kanuni za huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo Novemba, 2019;	300,000	Novemba, 2019	MOF, BOT, TCDC, LGA's
		(v) Sheria na Kanuni za huduma ndogo za fedha kutolewa kwa umma ifikapo Desemba, 2019;	300,000	Desemba, 2019	MOF, BOT, TCDC, LGA's

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(ii) Kuweka mkazo kwa watoa huduma ndogo za fedha kuzingatia kanuni za kuwalinda watumiaji wa huduma ndogo za fedha	(i) Kanuni za kumlinda mtumiaji wa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Juni, 2019; (ii) Mwongozo wa kumlinda mtumiaji wa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Juni, 2019;	150,000	Juni, 2019	MOFP, BOT, AGC, FCC TCRA, TCDC, LGA's
			300,000	Juni, 2019	MOFP, BOT, TCDC, FCC, MIVARF/ PMO, FSDT

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(iii) Kuweka mfumo wa sheria wa kubadilishana taarifa katika sekta ndogo ya fedha.	(i) Kanzidata ya sekta ya huduma ndogo za fedha kuanzishwa ifikapo Juni, 2019;	900,000	Juni, 2019	MOFP, BOT, TCDC, LGA's
		(ii) Kanuni kwa watoa huduma ndogo za fedha kutoa taarifa za wateja kwenye chombo cha kutunza taarifa za mikopo kuwekwa ifikapo Juni, 2019;	150,000	Juni, 2019	MOFP, BOT, TCDC, LGA's
		(iii) Elimu kwa Umma juu ya matumizi bora ya chombo cha kutunza taarifa za mikopo kutolewa ifikapo Novemba, 2019;	300,000	Novemba, 2019	MOFP/BOT
		(iv) Mfumo wa sheria na kanuni wa kubadilishana taarifa kati ya wasimamizi wa sekta ndogo ya fedha kuwekwa ifikapo Juni, 2019.	150,000	Juni, 2019	MOFP, BOT, TCDC, LGA's, TCRA

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
4. Kuongeza utafiti, ubunifu na uendelezaji wa huduma katika sekta ndogo ya fedha	(i) Kuongeza uwezo wa watunga sera na wadau wa sekta ndogo ya fedha kufanya tafiti.	(i) Programu za kujenga uwezo kwa watunga sera, wanataaluma, na wadau wengine katika huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2028	900,000	Juni, 2028	MOFP, BOT, FSĐT, Academic Institutions, MIVARE, Washirika wa Maendeleo
	(ii) Kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kufanya tafiti.	(ii) Utafiti wa kukuza sekta ndogo ya fedha kufanyika ifikapo mwaka 2028.	900,000	Juni, 2028	MOFP, BOT, FSĐT Academic Institutions, MIVARE, DPs
	(ii) Kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kufanya tafiti.	(i) Watafiti wa ndani kushiriki katika tafiti za kikanda na kimataifa za huduma ndogo za fedha ifikapo mwaka 2028;	300,000	Juni, 2028	MOFP, MFAEAIC, FSĐT Academic Institutions, MFIs

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(iii) Kuhamasisha ubunifu wa huduma ndogo za fedha.	(i) Mifuko ya ubunifu katika sekta ndogo ya fedha kuimarishwa ifikapo Juni, 2028	600,000	Juni, 2028	MOFP, FSĐT, COSTECH Academic Institutions, MFIs
		(ii) Shindano la mwaka la ubunifu wa huduma ndogo za fedha kufanyika ifikapo Juni, 2028.	900,000	Juni, 2028	MOFP, BOT, LGA's, TCDC, FSĐT Academic Institutions, MIVARE,
	(iv) Uenezaji na ubadilishanaji wa taarifa za matokeo ya utafiti kwa umma.	Matokeo ya utafiti kutolewa kwa umma ifikapo mwaka 2028.	540,000	Juni, 2028	MOFP, FSĐT Academic Institutions, MFIs

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
5. Kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwenye sekta ndogo ya fedha.	(i) Kuoanisha mfumo wa sera, sheria na kanuni kwa masuala ya huduma ndogo za fedha ya kulingana na ushirikiano wa kikanda na kimataifa.	(i) Tathmini katika sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha kwa kuzingatia mikataba na itifaki za kikanda na kimataifa kufanyika ifikapo mwaka 2020;	300,000	Juni, 2020	MOFP, BOT, MFAEAIC
		(ii) Mifumo ya sheria na kanuni kwenye sekta ndogo ya fedha kuoainishwa na viwango vya kikanda na kimataifa ifikapo 2020;	600,000	Juni, 2020	MOFP, AGC's, MFAEAIC, BOT
		(iii) Itifaki na makubaliano yanayohusiana na sekta ndogo ya fedha kuridhiwa ifikapo mwaka 2028;	600,000	Juni, 2028	MOFP, AGC's, MFAEAIC, TCDC, BOT and LGA's
		(iv) Kushiriki kwenye mikutano ya kikanda na kimataifa ifikapo mwaka 2028;	900,000	Juni, 2028	MOFP, AGC's, MFAEAIC, TCDC, BOT and LGA's

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(ii) Kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta ndogo ya fedha kwa jumuiya za kikanda na kimataifa.	(i) Mipango ya uelewa juu ya fursa zilizopo za uwekezaji kikanda na kimataifa kufanyika ifikapo mwaka 2028; (ii) Mikataba ya uwekezaji baina ya nchi wanachama na mashirika ya kimataifa kuhusu sekta ndogo ya fedha kujadiliwa ifikapo mwaka 2020; (iii) Miongozo ya ushirikiano kimipaka kwa wasimamizi wa sekta ndogo ya fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2020;	300,000	Juni, 2028	MOFP, MFAEAIC, BOT, TCDC
			600,000	Juni, 2020	MOFP, MFAEAIC, BOT, TCDC
			300,000	Juni, 2020	MOFP, MFAEAIC, BOT,TCDC

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(iii) Kuanzisha mtandao wa usimamizi kikanda kwa lengo la kusimamia udhibiti wa majanga na utatuzi wa migogoro.	(i) Mikataba ya Makubaliano baina ya mamlaka za usimamizi wa huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo 2019;	150,000	Juni, 2019	MOFP, MFAEAIC, BOT, MIVARF/PMO, MFIs
		(ii) Programu za uhamasishaji kwa ajili ya kuoanisha taratibu za mipaka na mamlaka nyingine za usimamizi kwa lengo la kuzingatia kanuni na viwango vya soko kufanyika ifikapo mwaka 2019.	300,000	Juni, 2019	MOFP, MFAEAIC BOT, TCDC

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
6. Kuhimiza uzingatiaji wa kanuni za utawala bora kwenye sekta ndogo ya fedha.	(i) Kuimarisha uwajibikaji, usawa na uwazi kwa wadau wote wa sekta ndogo ya fedha.	(i) Miongozo kuhusu utawala bora kwenye sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo mwaka 2017; (ii) Taasisi za huduma ndogo za fedha katika kuzingatia miongozo ya utawala bora kwenye sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha kufuatiliwa ifikapo mwaka 2028;	900,000	Juni, 2019	MOFP, BOT, AGC's, MIVARF/PMO, FSDT, TCDC, LGAs
			150,000	Juni, 2028	MOFP, BOT, AGC's, MIVARF/PMO, FSDT, TCDC, LGAs

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(ii) Kuweka mfumo wa sheria na kanuni kwa taasisi za huduma ndogo za fedha kutoa taarifa za vyanzo vya fedha kwa mujibu wa sheria ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu kwa sekta kutolewa ifikapo mwaka 2028.	(i) Mfumo wa Sheria na kanuni kwa taasisi za huduma ndogo za fedha kutoa taarifa za vyanzo vya fedha kwa mujibu wa sheria ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu kuwekwa ifikapo Juni, 2028 (ii) Elimu kuhusiana na udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu kwenye sekta ndogo ya fedha kutolewa ifikapo mwaka 2028.	200,000	Juni, 2028	MOFP, BOT, TCRA, FIU TCDC, LGA's
			600,000	Juni, 2028	MOFP, BOT, FIU TCDC, TCRA, LGA's

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
7. Kujumuisha masuala ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana huduma ndogo za fedha katika upatikanaji na utumiaji wa huduma ndogo za fedha zenye usawa na kwa gharama nafuu.	(i) Kutoa elimu kwa makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kuhusu huduma ndogo za fedha zilizopo.	(i) Programu za uhamasishaji wa makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana katika sekta ndogo ya fedha kutekelezwa ifikapo mwaka 2028;	300,000	Juni, 2028	MOHCDEC, MOFP, TCDC, LGAs, FSDI, MIVARF/PMO.
		(ii) Mafunzo ya ujasiriamali kwa makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kufanyika ifikapo mwaka 2028;	900,000	Juni, 2028	MOHCDEC, MOFP, TCDC, LGAs, FSDI, MIVARF/PMO.
		(iii) Makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kuhamasishwa kuunda makundi ya huduma za fedha ifikapo mwaka 2028;	900,000	Juni, 2028	MOFP, BOT, NEEC, TCDC, LGAs, MOHCDEC and

Lengo	Mkakati	Shabaha	Rasilimali (TZS '000)	Muda	Mhusika
	(ii) Kuhamasisha watoa huduma ndogo za fedha kuendeleza ubunifu kwenye utoaji wa huduma ili kukidhi mahitaji ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana.	(i) Huduma ndogo za fedha zinazokidhi mahitaji ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kutolewa ifikapo Juni, 2020;	300,000	Juni, 2020	MOHCDEC, MOFP, TCDC, LGAs, FSDI, MIVARF/PMO, Academic Inst, Media.
		(ii) Mfumo wa utoaji taarifa kwa kila kundi lenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kutoka kwa taasisi za huduma ndogo za fedha kuandaliwa ifikapo Juni, 2020.	120,000	Juni, 2020	MOHCDEC, MOFP, TCDC, LGAs, FSDI, MIVARF/PMO
Jumla Kuu			936,860,000		

SURA YA SITA

WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU WAKUU

Wizara inayohusika na masuala ya fedha ina jukumu na wajibu mkubwa wa kuhakikisha utekelezaji thabiti wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017, na Mkakati wa Utekelezaji wake kwa kushirikiana na wadau wengine katika sekta ya fedha. Wajibu na majukumu ya wadau wakuu ni kama ifuatavyo:

6.1 Wajibu na Majukumu ya wadau wa Huduma Ndogo za Fedha

Sera hii imezingatia changamoto, fursa na maendeleo mapya yaliyojitokeza, ikiwa ni pamoja na wajibu na majukumu ya watendaji na taratibu za uratibu na mahusiano yao. Watekelezaji wa Sera hii wanajumuisha Wizara mbalimbali za Serikali, Mamlaka za Umma, Sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo.

Serikali itahamasisha ukuaji wa sekta ndogo ya fedha kwa kiwango kikubwa kwa kushirikisha wadau wengine muhimu katika kuwezesha utekelezaji madhubuti wa Sera hii. Aidha, wajibu na majukumu ya Serikali kupitia Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali na taasisi mbalimbali yameainishwa kama ifuatavyo:

Wizara inayohusika na masuala ya fedha

Wizara inayohusika na masuala ya fedha itakuwa na jukumu la jumla la kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017. Wizara hii itahusika na:

- (i) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha;
- (ii) Kukuza shughuli za huduma ndogo za fedha nchini;
- (iii) Kuimarisha mfumo wa sheria na kanuni kwenye Sekta ndogo ya fedha;
- (iv) Kusimamia na kutathmini maendeleo ya sekta ya fedha ikijumuisha Sekta ndogo ya fedha;
- (v) Kuzuia utakasishaji wa fedha haramu;

- (vi) Kuundwa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa huduma ndogo za fedha;
- (vii) Kuratibu shughuli za Washirika wa Maendeleo kulingana na maelekezo ya Sera;
- (viii) Kuwezesha uundwaji wa chama kilele; na
- (ix) Kuandaa taarifa za sekta ndogo ya fedha.

Kitengo cha Huduma Ndogo za Fedha chini ya Wizara inayohusika na Masuala ya Fedha

Kitengo cha Huduma Ndogo za Fedha chini ya wizara inayohusika na masuala ya fedha kitakuwa na jukumu la kudhibiti na kusimamia taasisi za huduma ndogo za fedha.

Kitengo hiki kitahusika hasa na:

- (i) Kutoa leseni, kudhibiti na kusimamia taasisi za huduma ndogo za fedha zisizochukua amana;
- (ii) Kuendeleza na kusimamia kanzidata ya huduma ndogo za fedha nchini;
- (iii) Kufuatilia na kutathmini maendeleo ya Sekta ndogo ya fedha;
- (iv) Kuandaa kongamano la mwaka kwa watoa huduma ndogo za fedha; na
- (v) Kuandaa taarifa za Sekta ndogo ya fedha.

Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Sekta Ndogo ya Fedha

Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 inatoa nafasi ya kuanzisha Kamati ya usimamizi ya Taifa ya Sekta ya Huduma Ndogo za Fedha itakayojumuisha wajumbe kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Wizara inayohusika na masuala ya utumishi wa umma, Wizara inayohusika na masuala ya fedha; Benki Kuu ya Tanzania; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania; Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania; Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; Mamlaka ya Udhibiti wa Masoko ya Mitaji na Dhamana; na Chombo cha juu cha asasi/mitandao ya Watoa Huduma Ndogo za Fedha.

Kamati itakuwa na majukumu yafuatayo:

- (i) Kutumika kama chombo cha ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017;
- (ii) Kuhakikisha kunakuwepo na makubaliano kati ya Wizara mbalimbali na watendaji wengine kwenye hatua muhimu za kuboresha sekta ndogo ya fedha nchini na kufuatilia mafanikio ya hatua hizo;
- (iii) Kuishauri Serikali kwenye hatua sahihi za kutatua changamoto za sekta ndogo ya fedha; na
- (iv) Kuhamasisha uratibu wa pamoja wa sekta mbalimbali katika shughuli ndogo za fedha nchini.

Baraza la Wasimamizi wa Huduma Ndogo za Fedha

Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 inaelekeza uanzishawaji wa Baraza la Wasimamizi wa Huduma Ndogo za Fedha ambalo litakuwa na majukumu yafuatayo:

- (i) Kujenga muafaka kwa masuala ya maslahi ya pamoja katika sekta ndogo ya fedha;
- (ii) Kuandaa mazingira wezeshi katika kusaidia taasisi za huduma ndogo za fedha kubadilika kutoka daraja moja kwenda lingine;
- (iii) Kuoanisha mifumo ya sheria na kanuni; na
- (iv) Kufuatilia masuala yanayojitokeza kwenye sekta ndogo ya fedha, zikiwemo huduma mpya ili kuwezesha kufanyika kwa mapitio ya mifumo ya usimamizi iliyopo.

Wizara zinazohusika na Maendeleo ya Sekta Binafsi, Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Wizara inayohusika na maendeleo ya sekta binafsi, uwekezaji na uwezeshaji wa kiuchumi itatekeleza yafuatayo:

- (i) Kuweka mazingira ya sheria yanayotambulika na mfumo imara wa taasisi ambao utatumika kama motisha katika kupunguza gharama na kufanya biashara;
- (ii) Kuratibu uwekezaji (ukiwemo uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ya nchi) na ushirikiano kati ya sekta ya Umma na sekta binafsi;
- (iii) Kuimarisha ushirika wa sekta binafsi;
- (iv) Kuendelea kusimamia, kufuatilia na kuratibu mifuko na programu

- za Serikali zinazojihusisha na shughuli za huduma ndogo za fedha;
- (v) Kufuatilia na kutathmini mifuko na programu za Serikali;
 - (vi) Kuendeleza na kusimamia kanzidata ya mifuko na programu za Serikali; na
 - (vii) Kuandaa taarifa za mifuko na programu ya Serikali.

Wizara inayohusika na Masuala ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Wizara inayohusika na masuala ya tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa itatekeleza yafuatayo:

- (i) Kutoa miongozo na kufuatilia masuala ya huduma ndogo za fedha yaliyojumuishwa kwenye mipango na sheria ndogo za Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (ii) Kuendeleza na kusimamia kanzidata ya vikundi vya kifedha vya kijamii ; na
- (iii) Kuandaa taarifa za vikundi vya kifedha vya kijamii.

Tawala za Mikoa

Tawala za mikoa zitahusika na:

- (i) Kutoa miongozo na kufuatilia masuala ya huduma ndogo za fedha yalijumuishwa kwenye mipango na sheria ndogo za Serikali za mitaa;
- (ii) Kuratibu shughuli za huduma ndogo za fedha katika ngazi ya Mkoa; na
- (iii) Kuandaa taarifa za vikundi vya kifedha vya kijamii.

Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za serikali za mitaa zitahusika na:

- (i) Kusajili kusimamia na kudhibiti vikundi vya kifedha vya kijamii
- (ii) Kuendeleza na kusimamia kanzidata ya vikundi vya kifedha vya kijamii;
- (iii) Kuendelea kuhamasisha urasimishaji wa watoa huduma za fedha wasio rasmi;
- (iv) Kuanzisha Kamati ya Huduma ndogo za fedha;
- (v) Kufuatilia na kutathmini maendeleo ya watoa huduma za fedha kwenye vikundi; na

- (vi) Kuandaa taarifa za vikundi vya kifedha vya kijamii.

Wizara inayohusika na Elimu

Wizara inayohusika na masuala ya Elimu itahusika na:

- (i) Kuwezesha utoaji wa elimu ya huduma ndogo za fedha kwenye shule na vyuo.

Benki Kuu ya Tanzania

Benki Kuu ya Tanzania itahusika na:

- (i) Kuboresha mazingira ya benki na taasisi za fedha kwa ajili ya kusaidia sekta ndogo ya fedha;
- (ii) Kuendelea kutoa leseni, kusimamia na kudhibiti benki, taasisi za fedha zinazotoa huduma ndogo za fedha na benki za huduma ndogo za fedha;
- (iii) Kukuza na kusimamia kanzidata kwa benki, taasisi za fedha zinazotoa huduma ndogo za fedha na benki za huduma ndogo za fedha; na
- (iv) Kuandaa taarifa za benki, taasisi za fedha zinazotoa huduma ndogo za fedha na benki za huduma ndogo za fedha.

Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi

Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi litahusika na:

- (i) Kuratibu mifuko na programu za Serikali;
- (ii) Kusimamia na kutathmini mifuko na programu za Serikali;
- (iii) Kuanzisha na kusimamia kanzidata za mifuko na programu ya Serikali; na
- (iv) Kuandaa taarifa kwa vipindi tofauti kuhusu mifuko na programu za Serikali.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania itahusika na:

- (i) Kuboresha mazingira wezeshi kwa kampuni za bima kutoa huduma ndogo za bima;
- (ii) Kutoa leseni, kudhibiti na kusimamia watoa huduma ndogo za bima; na
- (iii) Kuandaa taarifa kwa vipindi tofauti za huduma ndogo za bima.

Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii itahusika na:

- (i) Kuboresha mazingira wezeshi kwa mifuko ya hifadhi ya jamii ili iweze kutoa mikopo ya jumla kwa taasisi za huduma ndogo za fedha;
- (ii) Kutoa leseni, kudhibiti na kusimamia mifuko ya hifadhi ya jamii; na
- (iii) Kuandaa taarifa kwa vipindi tofauti za huduma ndogo za pensheni.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana itahusika na:

- (i) Kuboresha mazingira wezeshi kwa watoa huduma ndogo za fedha kupata mitaji kupitia masoko ya mitaji; na
- (ii) Kuandaa taarifa kwa vipindi tofauti za masoko ya mitaji.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania itahusika na:

- (i) Kusajili, kutoa leseni, kudhibiti na kusimamia Vyama vya Ushirika wa Kuweka Akiba na Mikopo (SACCOS) nchini;
- (ii) Kuratibu vyama vya ushirika katika kupata na kutumia huduma za fedha;
- (iii) Kuandaa na kusimamia kanzidata ya SACCOS;
- (iv) Kuhamasisha maendeleo ya SACCOS;
- (v) Kufuatilia na kutathmini SACCOS ; na
- (vi) Kuandaa taarifa kwa vipindi tofauti za SACCOS.

Watoa huduma ndogo za fedha

Watoa huduma ndogo za fedha watahusika na:

- (i) Kuzingatia mfumo wa sheria na kanuni wa Sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha pamoja na sheria nyingine zinazohusiana;
- (ii) Kuanzisha na kubuni huduma zinazokidhi mahitaji ya wananchi wa kipato cha chini;
- (iii) Kutoa elimu ya fedha na kuzingatia mfumo wa sheria na kanuni za kuwalinda walaji; na
- (iv) Kuandaa taarifa ya huduma ndogo za fedha kwa vipindi tofauti kama zitakavyohitajika na wasimamizi.

Watoa Huduma za Mifumo ya Malipo

Watoa huduma za mifumo ya malipo watahusika na:

- (i) Kuzingatia mfumo wa sheria na kanuni za sekta ndogo ya fedha pamoja na kanuni nyingine zinazohusiana;
- (ii) Kuanzisha mfumo wa kusambaza huduma ndogo za fedha kwa watoa huduma ndogo za fedha kwa njia ya kielektroniki; na
- (iii) Kutoa misaada ya fedha kwa ajili ya maendeleo ya sekta ndogo ya fedha.

Chama Kilele

Chama Kilele kitahusika na:

- (i) Kuzingatia mfumo wa sheria na kanuni wa sekta ndogo ya fedha pamoja na sheria nyingine zinazohusika;
- (ii) Kuandaa miongozo ya maadili kwa ajili ya shirikisho na ushirika wa huduma ndogo za fedha kwa kuendana na taratibu zinazokubalika kimataifa;
- (iii) Kusajili shirikisho na ushirika wa wanachama wa huduma ndogo za fedha;
- (iv) Kuanzisha na kusimamia kanzidata ya wanachama wa ushirika wa huduma ndogo za fedha;
- (v) Kuandaa taarifa za shirikisho na ushirika wa huduma ndogo za fedha kwa vipindi tofauti;
- (vi) Kuandaa programu za kujenga uwezo wa shirikisho na ushirika wa huduma ndogo za fedha; na
- (vii) Ushawishi na utetezi kwa niaba ya shirikisho na ushirika wa watoa huduma ndogo za fedha.

Washirika wa Maendeleo:

Washirika wa maendeleo watawajibika na:

- (i) Kuzingatia mfumo wa sheria na kanuni za sekta ndogo ya fedha na sheria nyingine zinazohusiana; na
- (ii) Kutoa msaada wa kitaalam na fedha kwa sekta ndogo ya fedha.

Taasisi za Taaluma:

Taasisi za taaluma zitahusika na:

- (i) Kuandaa na kuendesha mafunzo kulingana na mahitaji ya uendeshaji wa huduma ndogo za fedha;
- (ii) Kuendesha mafunzo ya muda mfupi, wa kati na mrefu yanayoendana na mitaala ya elimu ya taifa ya huduma ndogo za fedha; na
- (iii) Kufanya utafiti kuhusu Sekta ndogo ya fedha.

Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari vitahusika na:

- (i) Kueneza shughuli za huduma ndogo za fedha ikiwa ni pamoja na kuhamasisha elimu ya huduma za fedha; na
- (ii) Kujenga uelewa wa umma kuhusu huduma zinazotolewa na sekta ndogo ya fedha.

Watoa Huduma wa Kuwezesha Maendeleo ya Biashara

Watoa huduma wa kuwezesha maendeleo ya biashara watawajibika na:

- (i) Kuzingatia mfumo wa sheria na kanuni za sekta ndogo ya fedha na sheria nyingine zinazohusiana;
- (ii) Kutoa msaada wa fedha kwa ajili ya kuendeleza sekta ndogo ya fedha;
- (iii) Kutoa huduma za kuendeleza ujuzi wa biashara kwa wateja wa huduma ndogo za fedha na watoa huduma ndogo za fedha ; na
- (iv) Kuandaa taarifa ya huduma ndogo za fedha kwa vipindi tofauti kama zitakavyohitajika na mamlaka za usimamizi.

SURA YA SABA

MFUMO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI

7.1 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni utaratibu unawekwa kwa ajili ya kupima maendeleo na kutathmini kiwango cha malengo mahususi yaliyofikiwa kwa kulinganisha na malengo yaliyopangwa. Ufanisi katika mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unategemea uratibu mzuri na utendaji kwa kila daraja kuanzia ukusanyaji wa taarifa hadi uchambuzi na utoaji wa taarifa kwa wadau wote husika.

Jukumu la ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017 lipo chini ya wizara inayohusika na masuala ya fedha. Wizara itakuwa na jukumu la uratibu, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Sera hii. Ili kuwa na ufanisi katika kutathmini na ufuatiliaji, kila mdau atakuwa na wajibu wa kuanzisha mfumo wa ndani wa ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa kuna uwezo wa kutathmini na kupima ufanisi na utendaji katika taasisi husika kuhusiana na Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017.

Ufuatiliaji na tathmini utahusisha pamoja na mambo mengine, kufanya utafiti wa awali, kutengeneza viashiria vya utendaji na kuweka mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Ufuatiliaji wa maendeleo ya utekelezaji wa hatua na malengo yaliyofikiwa utafanyika kwa vipindi tofauti. Aidha, kutakuwa na mapitio ya kila mwaka, ambayo yatalenga kupima endapo shughuli zilizopangwa zinaendana na mafanikio ya malengo yaliyowekwa. Vile vile, mapitio yatahusisha kufanya tafiti za aina mbalimbali kwa walengwa na kufuatilia mabadiliko yaliyojitokeza kutokana na matokeo yaliyopatikana katika kipindi cha mapitio.

7.2 Malengo na miongozo ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

7.2.1 Malengo ya Jumla na Mahsusi

Lengo kuu la mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni kutoa mwongozo wa utekelezaji wa Sera na mkakati wake kwa lengo la kufikia ufanisi wa kiwango cha juu na wenye tija. Mfumo huu unalenga hususan:

- (i) Kuweka vigezo vya viashiria vya tathmini ya sera na programu;
- (ii) Kuweka shabaha na vigezo vya utekelezaji wa sera;
- (iii) Kuelekeza wadau katika shughuli za utekelezaji na ufuatiliaji; na
- (iv) Kudhibiti matumizi ya rasilimali wakati wa utekelezaji.

7.2.2 Miongozo ya Tathmini na Ufuatiliaji

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha utakuwa chini ya miongozo ifuatayo:

- (i) Kuoanisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na mifumo mingine ya Serikali;
- (ii) Kuoanisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na mifumo mingine ya Washirika wa Maendeleo;
- (iii) Kutumia mfumo wa utendaji wenye misingi ya matokeo;
- (iv) Tathmini na ufuatiliaji ioneshe hali ilivyo;
- (v) Kujenga uwezo katika shughuli za ufuatiliaji na tathmini; na
- (vi) Kupitia mfumo wa ufuatiliaji na tathmini mara kwa mara.

7.3 Wigo wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utajumuisha yafuatayo:

- (i) Kupima mchango, mchakato na matokeo ya utekelezaji wa Sera;
- (ii) Kanzidata na mfumo wa kutoa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya Sera; na
- (iii) Ufuatiliaji wa mipango na utekelezaji, ikijumuisha utekelezaji wa kifedha na halisi.

7.3.1 Viashiria vya utekelezaji

Wizara inayohusika na masuala ya fedha itatumia viashiria vilivyoandaliwa kwa kuzingatia dhima, malengo na matokeo ya Sera. Hii ni pamoja na yafuatayo:

Jedwali 7.1: Viashiria vya Utekelezaji katika mfumo wa Tathmini na ufuatiliaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha.

Malengo ya Mkakati	Kiashiria cha Utekelezaji	Kiashiria cha Matokeo	Msingi	Chanzo
Lengo la Mkakati 1: Kuhamasisha ukuaji wa sekta ya fedha iliyo imara na jumuishi	(i) Idadi ya watu binafsi, kaya na shughuli za biashara ambazo zimepata huduma za fedha	(i) Uwiano wa huduma ndogo za fedha zilizoenea vijijini.	65%	Ripoti ya Finscope (2017) Ripoti ya utafiti wa mapato na matumizi ya Kaya (2011/2012)
	(ii) Idadi ya watu binafsi, kaya na shughuli za biashara zilizopatiwa huduma za ugani.	(ii) Ukuaji wa soko la huduma ndogo za fedha.		
	(iii) Idadi ya vipindi vya elimu ya huduma ndogo za fedha vilivyotolewa	(iii) Asilimia ya idadi na thamani ya mikopo iliyotolewa kwenye shughuli za kilimo		
	(iv) Idadi ya watu binafsi, kaya na shughuli za biashara zilizopata huduma za ubunifu	(iv) Ongezeko la tija kwa eneo la mraba		
	(v) Idadi ya wajasiriamali wadogo na wa kati wanaopata misaada ya Serikali.	(v) Ongezeko la matumizi kwa mtu kwenye kikundi kidogo.		

Malengo ya Mkakati	Kiashiria cha Utekelezaji	Kiashiria cha Matokeo	Msingi	Chanzo
	<p>(vi) Idadi ya mazao yanayozalishwa kwa mfumo wa kilimo cha mkataba</p> <p>(vii) Idadi ya maghala yanayotumia mfumo wa stakabadhi za mazao.</p> <p>(viii) Idadi ya wasindikaji wa mazao wanaopata huduma za fedha</p> <p>(ix) Idadi ya wafanyabiashara wa bidhaa na wasafirishaji wanaopata huduma za fedha.</p>	<p>(vi) Idadi na thamani ya bidhaa zilizouzwa.</p> <p>(vii) Asilimia ya idadi na thamani ya mikopo iliyoelekezwa kwenye mnyororo wa thamani wa kilimo</p> <p>(viii) Asilimia ya ushirika wa wakulima na vyama vya ushirika wa kuuza mazao vilivyopata mkopo kutoka kwa Taasisi za huduma ndogo za fedha</p> <p>(ix) Asilimia ya utumiaji wa huduma za fedha kwa njia ya mtandao wa simu iliongezeka</p>		

Malengo ya Mkakati	Kiashiria cha Utekelezaji	Kiashiria cha Matokeo	Msingi	Chanzo
	<p>(x) Idadi ya hati za ardhi na mali zilizosajiliwa.</p> <p>(xi) Idadi ya watu binafsi, kaya na shughuli za biashara ambazo zimepata huduma za fedha baada ya kurasimisha mali na biashara.</p> <p>(xii) Aina ya huduma za fedha kwa ajili ya nyumba zinazowalenga wananchi wenye kipato cha chini.</p>	<p>(x) Asilimia ya makazi yaliyoboreshwa maeneo ya vijijini.</p> <p>(xi) Asilimia ya Wananchi wenye kipato cha chini wanaopata huduma ndogo za mikopo ya nyumba</p> <p>(xii) Idadi ya Ubia kati Sekta ya Umma na Binafsi katika kutoa huduma kwenye sekta ndogo ya fedha</p>		
<p>Lengo la Mkakati 2: Kuwa na uendeleu kwa watoa huduma ndogo za fedha.</p>	<p>(i) Idadi ya watoa huduma wa jumla katika sekta ndogo za fedha.</p> <p>(ii) Idadi ya taasisi za huduma ndogo za fedha zilizoboreshwa</p> <p>(iii) Idadi ya taasisi za huduma ndogo za fedha zinazopata mitaji kwa njia ya dirisha la EGM</p> <p>(iv) Uwiano wa uwekaji akiba</p>	<p>(i) Kiwango cha mikopo kwa wateja wa vijijini</p> <p>(ii) Kiasi cha Mtaji kilicho patikana kupitia dirisha la EGM.</p>	N/A	MOFP, BOT, CMSA,

Malengo ya Mkakati	Kiashiria cha Utekelezaji	Kiashiria cha Matokeo	Msingi	Chanzo
	<p>(v) Idadi ya vikundi vya kifedha vya kijamii vilivyou nganishwa na taasisi za huduma ndogo za fedha na benki.</p> <p>(vi) Idadi ya taasisi za huduma ndogo za fedha na wateja waliopata mafunzo</p>			
<p>Lengo la Mkakati 3: Kuweka mfumo wa sheria na kanuni ili kuongeza ufanisi kwenye utoaji wa huduma ndogo za fedha.</p>	<p>(i) Kuwepo kwa Sheria ya Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha</p> <p>(ii) Kuanzishwa kwa Chombo cha juu cha asasi/mitandao ya Watoa Huduma Ndogo za Fedha</p> <p>(iii) Kuwepo kwa Kanuni za utendaji kwa muungano wa taasisi za taasisi za huduma ndogo za fedha</p> <p>(iv) Kuanzisha utaratibu wa kupima taasisi za huduma ndogo za fedha</p>	<p>(i) Kuwepo kwa taarifa za taasisi za huduma ndogo za fedha zenye kuaminika, sahihi na zinazotolewa kwa wakati</p> <p>(ii) Idadi ya taasisi za huduma ndogo za fedha zilizopimwa.</p> <p>(iii) Uwiano wa ujumuishwaji kwenye huduma za fedha</p>	N/A	AGC,PO-RALG MOFP, TCDC, MFI's Apex Body

Malengo ya Mkakati	Kiashiria cha Utekelezaji	Kiashiria cha Matokeo	Msingi	Chanzo
Lengo la Mkakati 4: Kukuza utafiti, ubunifu na uendelezaji wa huduma kwenye sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha.	(i) Idadi ya tafiti zilizofanyika (ii) Kuboreka kwa huduma katika sekta ndogo ya fedha; na (iii) Kuboresha elimu na uelewa juu ya masuala ya huduma ndogo za fedha	Asilimia ya ongezeko la wataalamu wa ndani wa huduma ndogo za fedha.		MOFP, FSDT Academic Institutions, MFIs

Malengo ya Mkakati	Kiashiria cha Utekelezaji	Kiashiria cha Matokeo	Msingi	Chanzo
<p>Lengo la Mkakati 5: Kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwenye sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha.</p>	<p>(i) Mifumo ya kisheria na kanuni katika sekta ya huduma ndogo za fedha kuzingatia viwango vya kikanda na kimataifa.</p> <p>(ii) Kuwepo kwa kamati ya kitaifa ya Watalaam kuhusu ushirikiano wa kikanda na kimataifa</p> <p>(iii) Kanuni, itifaki, mikataba, nyaraka za maelewano na mikataba ya utoaji huduma ya kikanda na kimataifa, kuridhiwa na Serikali</p>	<p>(i) Kuongezeka kwa misaada kutoka nje ya nchi kwenye sekta ndogo ya fedha</p> <p>(ii) Kuongezeka kwa idadi ya taasisi za huduma ndogo za fedha mipakani</p> <p>(iii) Kuongezeka kwa kiwango na thamani ya huduma za taasisi ndogo za fedha mipakani</p> <p>(iv) Kuimarika kwa ubadilishanaji uzoefu na ujuzi kwenye masuala ya huduma ndogo kikanda na kimataifa.</p> <p>(v) Idadi ya ushirikiano wa kimataifa na kikanda wa kuongeza wigo wa huduma ndogo za fedha nchini.</p>	N/A	MOFP

Malengo ya Mkakati	Kiashiria cha Utekelezaji	Kiashiria cha Matokeo	Msingi	Chanzo
Lengo la Mkakati 6: Kuhimiza uzingatiaji wa kanuni za utawala bora kwenye sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha.	<p>(i) Miongozo ya kuhimiza utawala bora kwenye sekta ya huduma ndogo za fedha kuandaliwa</p> <p>(ii) Idadi ya taasisi za huduma ndogo za fedha kuendana na kanuni za udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu</p>	(i) Idadi ya watendaji wanaotekeleza miongozo	N/A	MOFP, BOT, TCDC, PO-RALG and Microfinance Apex Body

Malengo ya Mkakati	Kiashiria cha Utekelezaji	Kiashiria cha Matokeo	Msingi	Chanzo
Lengo la Mkakati 7: Kujumuisha masuala ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana katika upatikanaji na utumiaji wa huduma ndogo za fedha zenye usawa na gharama nafuu.	<ul style="list-style-type: none"> (i) Idadi ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kupata huduma ndogo za fedha (ii) Kiwango cha elimu iliyotolewa kwenye masuala ya huduma ndogo za fedha (iii) Taarifa ya uchambuzi wa masuala ya jinsia. (iv) Miongozo kwa ajili ya kujumuisha masuala ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana kwenye huduma ndogo za fedha. 	(i) Kiwango cha watoa huduma ndogo za fedha waliojumuisha masuala ya makundi yenye mahitaji maalum, jinsia na vijana.	N/A	MOFF, BOT, TCDC, PO-RALG and Microfinance Apex Body

7.4 Ukusanyaji na Uchambuzi wa Takwimu

Takwimu kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini zitakusanywa mara kwa mara kwa kutumia njia sahihi kama ilivyokubaliwa katika Mamlaka ya Taifa ya Uratibu. Takwimu zitakusanywa kupitia dodoso, tafiti, taarifa za utendaji za mara kwa mara, ziara za ufuatiliaji na mbinu nyingine za kuaminika zenye taratibu na vyanzo sahihi. Takwimu zitachambuliwa ipasavyo na kuingizwa katika mfumo wa kompyuta wa taifa wa huduma ndogo za fedha zinazotolewa kwa mujibu wa Sera hii. Kadhalika, kuanzishwaji kwa benki ya takwimu kutawezesha upatikanaji wa takwimu zinazohitajika kwa ajili ufuatiliaji na tathmini.

7.4.1 Aina ya taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Katika ngazi ya taasisi, taarifa mbalimbali zitatumiwa kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini kama ifuatavyo:

- (i) Taarifa ya Wizara ya Fedha na Mipango ya nusu-mwaka na ya mwaka;
- (ii) Taarifa ya tathmini ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Mashirika ya kikanda na Halmashauri za Serikali za Mitaa;
- (iii) Taarifa za kila mwaka za Washirika wa Maendeleo; na
- (iv) Taarifa mbalimbali za mapitio, tafiti na dodoso.

Jedwali Na. 7.2: Aina ya Taarifa

Aina ya Taarifa	Yaliyomo	Muda
Taarifa za kina za utendaji	Taarifa inayojumuisha kazi zote zilizofanyika katika ngazi zote za kitaasisi	Robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima
Taarifa ya utekelezaji wa mali/vifaa na fedha	Utekelezaji halisi, mapato na matumizi	Robo mwaka, nusu mwaka na mwaka
Tathmini/taarifa ya maendeleo	Taarifa ya tathmini ya ndani na nje kuhusu Programu	Mwaka, miaka miwili, miaka mitatu au mitano
Tathmini ya Sera	Mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha.	Baada ya miaka mitano

7.4.2 Ratiba ya Utoaji Taarifa

Jedwali No. 3 linaonyesha ratiba pamoja na mambo ya kuzingatia kwenye utoaji taarifa:

Jedwali 7.3: Ratiba ya Utoaji Taarifa ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Sera

Aina ya ripoti	Yaliyomo	Muda
1. Taarifa ya huduma ndogo za fedha	Taarifa ya kina inayojumuisha viashiria muhimu vya huduma ndogo za fedha vilivyoainishwa katika Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017	Kila mwaka
2. Taarifa za Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala	Taarifa za utendaji kwenye utekelezaji wa masuala ya huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sera	Nusu mwaka, kila mwaka
3. Taarifa za Halmashauri za Serikali za Mitaa	Taarifa za kiutendaji kwenye utekelezaji wa masuala ya huduma ndogo za fedha katika Halmashauri za Serikali za Mitaa	Robo mwaka, nusu mwaka, kila mwaka
4. Taarifa za Washirika wa Maendeleo	Taarifa za kitaalam, uwezesaji, taratibu za kiutendaji na aina nyingine ya misaada iliyotolewa, ikijumuisha maeneo ya kijiografia (mikoa) na makundi ya walengwa	Kila mwaka, nusu mwaka
5. Taarifa za taasisi zisizo za kiserikali (sekta binafsi, bodi na wadau wengine)	Taarifa za utendaji kwenye utekelezaji wa masuala ya huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sera	Nusu mwaka, mwaka

6. Taarifa za Ukaguzi za taasisi za huduma ndogo za fedha	Matokeo ya kaguzi kuhusu shughuli za taasisi za huduma ndogo za fedha.	Robo mwaka, miezi sita, Mwaka
7. Taarifa za tafiti kuhusu taasisi za huduma ndogo za fedha.	Hizi ni pamoja na tafiti za Kaya, na tafiti nyingine maalum.	Inaweza kuwa mara kwa mara au pindi itakapohitajika
8. Mapitio ya matumizi ya Serikali kwenye shughuli za taasisi za huduma ndogo za fedha	Kufuatilia na kuchambua mgawanyo wa rasilimali, matumizi	Kila baada ya miaka miwili
9. Taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Sera na Mkakati	Uchambuzi kwa njia ya uwazi wa matokeo ya maazimio yaliyotekelezwa.	Muda wa kati (Baada ya miaka 5) na kipindi cha mwisho (baada ya miaka 10)
10. Taarifa ya tathmini ya Mpango/ Programu	Uchambuzi kwa njia ya uwazi wa matokeo ya maazimio ya utekelezaji wa Programu na miradi nchini ambayo kwa kiwango kikubwa yamefanikisha malengo ya Sera na Mkakati.	Taarifa kwa kipindi cha muda wa kati na wa mwisho kwa kuzingatia ratiba.

7.4.3 Mtiririko wa Utoaji Taarifa

Taarifa kuhusu mafanikio ya malengo na viashiria zitaandaliwa na taasisi husika na kuwasilishwa Wizara inayohusika na masuala ya fedha kufanyiwa majumuisho. Wizara inayohusika na masuala ya fedha itaandaa taarifa jumuisi katika vipindi vya robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima kwa ajili ya kusambazwa kwa wadau wote kwa ajili ya kumbukumbu na hatua muhimu.

7.4.4 Mfumo wa Utoaji Mrejesho

Mfumo wa utoaji mrejesho umeweka njia mbili za mtiririko wa taarifa baina ya watayarishaji na watumiaji, maoni yanapaswa kujumuishwa kwenye mwingiliano uliopo miongoni mwa wadau ili kuongeza ubora na uwasilishaji wa taarifa.

7.5 Matumizi ya Taarifa za Tathmini na Ufuatiliaji

Taarifa za tathmini na ufuatiliaji zitatumiwa na Serikali, Washirika wa Maendeleo, walengwa na wadau wengine kwa:

- (i) Kutoa huduma bora;
- (ii) Kutoa matokeo kama sehemu ya uwajibikaji;
- (iii) Kufanya maamuzi;
- (iv) Kupanga; na
- (v) Kugawa rasilimali.

7.6 Mpango wa Utekelezaji

Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017 utakaokuwa na vipaumbele saba vya kiseru kama vilivyoainishwa katika Sera na Mkakati utaandaliwa baada ya kuidhinishwa kwa Sera. Mikakati iliyotajwa imebainisha hatua zitakazochukuliwa, kazi zitakazofanyika na makadirio ya gharama zake. Sekta zote na watendaji watapaswa kuzingatia Mpango Kazi uliotengenezwa kwa njia shirikishi na jumuishi, na hivyo kuwa msingi wa kuwa na mfumo wa kupima matokeo kwa lengo la kufikia malengo ya kutoa huduma ndogo za fedha kwa wananchi wenye kipato cha chini na wasiofikiwa na huduma hizi katika muda mfupi iwezekanavyo.